# Nipashe

Jumatatu Januari 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580457

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## CPB yaanza kurejesha mkopo wa bil. 3.6/- za NSSF

UKURASA 3



## Mwalimu adaiwa kumbaka mwanafunzi ofisini

UKURASA 4




UKURASA 11

# Ziara za mawaziri zilivyoibua 'madudu'

UKURASA 2



Baadhi ya wafanyabiashara ndogo ambao walihamishwa eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam kwa ajili ya ujenzi wa barabara, hivi sasa wamerejea na kujenga vibanda vyao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwinyi kuongoza Wazanzibari Mapinduzi

UKURASA 2

## TMA yatahadharisha mvua kubwa yenye upepo

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

**MICHEZO** SIMBA YAMREJESHA MORRISON DIMBANI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6

# Ziara za mawaziri zilivyoibua 'madudu'

**Na Thobias Mwanakatwe**

KASI ya ziara za mawaziri na manaibu mawaziri katika maeneo mbalimbali nchini zimeibua 'madudu' ukiwamo ubadhirifu na uzembe kwa baadhi ya watendaji katika mikoa na wilaya walizotembelea.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili wa kufuatilia ziara za mawaziri hao ambazo wamezianza tangu walipoapishwa na Rais John Magufuli, umebaini kuibuliwa kwa 'madudu' mengi ambayo yalikuwa hayajafanyiwa kazi na viongozi wa serikali ngazi ya mkoa na wilaya.

Hata hivyo, hakuna sababu za wazi kwa baadhi ya viongozi wa serikali ngazi ya mikoa na wilaya kushindwa kuibua 'madudu' au kero na kuchukua hatua kumaliza matatizo kwenye maeneo yao.

Baadhi ya wakuu wa mikoa wameripotiwa katika vyombo vya habari wakionekana kuchukua hatua katika maeneo yao wanapobaini ubadhirifu na uzembe kwa watumishi walio chini yao, huku katika maeneo mengine hali hiyo hubainika baada ya viongozi wa juu kutembelea.

Mfano wa baadhi ya wakuu wa mikoa hao ni Mkuu wa Mikoa wa Mbeya, Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera na Mkuu wa Mkoa Morogoro, Loata Ole Sanare, ambao wameonekana kuchukua hatua baada ya kubaini kero mbalimbali katika maeneo yao.

Baadhi ya viongozi ambao wametikisa katika ziara zao mikoani ni pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ambaye katika ziara yake wilayani Sengerema alishtukia wizi wa mamilioni wa makusanyo ya mapato ya ndani katika Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema, mkoani Mwanza.

Waziri Jafo aliabini Sh. milioni 350 zimetafunwa na watumishi wa halmashauri hiyo.

Kadhalika, Naibu Waziri wa TAMISEMI, David Silinde naye katika ziara yake aliibua ubadhirifu katika Wilaya ya Singida.

Silinde alibaini ubadhirifu katika ujenzi wa bwalo la Sekondari ya Ikhanoda, wilayani humo na zaidi ya Sh. milioni 50 kutumika huku ujenzi ukiwa hatua ya msingi. Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, akiwa katika ziara mkoani Rukwa alibaini wizi wa dawa katika Hospitali ya Mkoa wa Rukwa, zenye thamani ya Sh. 9,600,000.

Kwa upande wa Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, katika ziara yake mikoa ya Mbeya na Songwe alibaini ubadhirifu na uzembe wa watendaji katika Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira hali ambayo imesababisha miradi ya maji kukwama na kusababisha kilio cha wananchi kukosa huduma hiyo kwa muda mrefu.

Kadhalika, Waziri wa Maji, Juma Aweso, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi katika ziara zao mikoani, wamekumbana na 'madudu' ya ubadhilifu katika miradi mbalimbali. Hata hivyo, wananchi wamekuwa wakijiuliza watendaji katika maeneo hayo ambao wote ni wateule wa rais wanashindwa vipi kuchukua hatua mpaka wanapofika mawaziri na manaibu wao.




Abiria wanaoelekea Wilaya ya Mbinga na Nyasa mkoani Ruvuma wakiwa katika kituo cha mabasi Ruhuwiko, Manispaa ya Songea, ambacho hakina sehemu ya kupumzikia abiria. **PICHA: MICHAEL EMMANUEL**

# Rais wa Msumbiji kuwasili nchini leo

**Na Elizabeth Zaya**

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, anatarajia kuwasili nchini leo kwa ziara ya kikazi ya siku mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari ujio wa rais huyo, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema Rais Nyusi atapokelewa na mwenyeji wake, Rais John Magufuli, wilayani Chato mkoani Geita.

Prof. Kabudi, alisema ziara hiyo ni ya kindugu ambayo ilipangwa kufanyika mwaka jana, lakini ilishindikana kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uchaguzi mkuu uliofanyika, mwaka jana.

"Kwa hiyo, ndiyo imekuwa wakati muafaka sasa wa kufanyika kwa ziara hiyo. Na kwa sababu inafanyika wakati ambapo Rais yupo Chato, basi amemkaribisha afike hapo," alisema Prof. Kabudi.

Alisema ziara hiyo ni kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha uhusiano wa nchi hizo mbili katika maeneo anuwai, yakiwamo ya diplomasia, kiuchumi, kisiasa na kijamii kama yalivyoasisiwa na vyama vya ukombozi vya nchi hizo.

Prof. Kabudi alisema: "Uhusiano huo uliyotukuka kati ya nchi hizi mbili uliasisiwa na viongozi waanzilishi wa nchi zetu hizi mbili."

Alisema uhusiano huo umeendelea kuimarika na Tanzania inafanya biashara na Msumbiji kupitia mazao ya chakula na ya viwandani.

"Kwa mujibu wa takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mauzo ya nje kati ya nchi hizi mbili yalifikia Sh. bilioni 76.4 mwaka 2018 na Sh. bilioni 93.5 mwaka 2019," alisema Prof. Kabudi.

Alisema licha ya changamoto ya mlipuko wa ugonjwa wa corona, lakini nchi hizo mbili zimeendelea kuwezesha na kusimamia biashara kati ya pande hizo.

"Kwa hiyo wakati wa ziara hii, viongozi wetu watabadilishana mawazo ya namna ya kuendeleza na kuwezesha ufanyaji wa biashara, lakini namna ya kuongeza idadi wa Watanzania wanaowekeza ndani ya Msumbiji na watu wa nchi hiyo wanaowekeza ndani ya Tanzania," alisema Prof. Kabudi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Geita, Robert Gabriel, alisema rais huyo anatarajia kuwasili majira ya asubuhi na kuwaomba wananchi wa mkoa huo kujitokeza kwa wingi kumpokea.

Gabriel alisema ni bahati kubwa kwa Tanzania kutembelewa na viongozi wakubwa katika kipindi kifupi katika Mkoa wa Geita, na kubainisha kwamba ni fursa pekee ya kutangaza mkoa huo, na kuwataka wakazi wake kuchangamkia fursa hiyo.

# Dk. Mwinyi kuongoza Wazanzibari Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kesho anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sherehe hizo zinatarajia kufanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana Mustafa, ilieleza kwamba siku hiyo Dk. Mwinyi, atawahutubia wananchi kupitia vyombo vya habari.

Pia ilieleza kuwa sherehe hizo zitaambatana na maandamano ya Mapinduzi yatakayowashirikisha vijana kutoka Unguja na Pemba, ambayo yataanzia katika Uwanja wa Matumbaku Miembeni hadi Uwanja wa Mnazi Mmoja, Kikwajuni Mjini Unguja.

Vilevile, ilieleza katika sherehe hizo, Dk. Mwinyi atapokea maandamano hayo pamoja na maonyesho ya vikosi vya ulinzi na usalama.

"Katika sherehe hizo viongozi mbalimbali watahudhuria wakiwamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wa vyama vya siasa, mabalozi pamoja na wananchi wa Zanzibar," alisema Mustafa.

Kadhalika, Mustafa alisema sherehe za mwaka huu zitakuwa za kwanza tangu Serikali ya Awamu ya Nane inayoongozwa na Dk. Mwinyi iingie madarakani Novemba, mwaka jana na kuwataka wananchi kuhudhuria kwa wingi.

Mustafa ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa mkoa huo, alisema vyombo vya ulinzi na usalama vimejipanga vizuri ili kuhakikisha hali ya amani inaimarika wakati wote wa sherehe hizo.

Aliwaomba wananchi kuhudhuria kwa wingi katika viwanja vya Maisara usiku Januari 11 (leo), kwa ajili ya kuangalia shamrashamra za maadhimisho ya sherehe hizo na mgeni rasmi siku hiyo anatarajiwa kuwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdalla.

Mustafa aliwapongeza wafanyakazi wa taasisi za serikali na binafsi na wananchi mbalimbali kwa kushiriki katika usafi wa mazingira, mashindano ya michezo, tamasha la biashara, ufunguzi na uwekaji wa mawe ya msingi miradi ya maendeleo.

# CPB yaanza kurejesha mkopo wa bil. 3.6/- za NSSF

**Na Mwandishi Wetu**

JUHUDI za Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) kuwekeza kwenye viwanda zimewavutia Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe.

Mawaziri hao walikuwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa uwekezaji uliofanywa na NSSF kwa kutoa mkopo wa Sh. bilioni 3.6 kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), jijini Dodoma, mwishoni mwa wiki.

Waziri Mhagama alisema NSSF kutoa mkopo kwa CPB kunalenga kuunga mkono juhudi za serikali katika kukuza uchumi wa nchi kupitia viwanda na uwekezaji huo utatoa soko la mazao, kuzalisha bidhaa ambazo zinahitajika nchini kupata fedha za kigeni na kutoa ajira kwa Watanzania. Mhagama aliitaka CPB kuhakikisha inarejesha mkopo huo kwa mujibu wa mkataba.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa CPB, Dk. Anslem Moshi, alimthibitishia Waziri Mhagama kwamba kwa upande wao wamejipanga kuhakikisha wanazalisha mazao bora ya biashara yalioongezwa thamani baada ya kupokea mkopo kutoka NSSF wa Sh. bilioni 3.6 ambao umewezesha kufufua kiwanda hicho na kununua mashine zenye ubora za kusaga unga na kuzalisha mafuta ya alizeti. Mafanikio hayo yamewezesha CPB kuanza kufanya marejesho ya mkopo waliochukua mwaka 2017 kutoka NSSF na Dk. Moshi alimwambia Waziri Mhagama kuwa wameanza kufanya marejesho ya Sh. milioni 400 mwezi Septemba 2020.

Naye Naibu Waziri Bashe, aliishukuru NSSF kwa mkopo waliotoa kwenye viwanda hivyo na atahakikisha anasimamia kwa karibu marejesho ya mkopo huo baada ya NSSF na CPB kuja na mpango bora zaidi wa watakavyofanya marejesho kwa upande wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko na vilevile NSSF iangalie namna bora ya kutoa riba nafuu ili kurahisisha marejesho hayo.

"Nipende kuwahakikishia NSSF pesa yenu itarudi, tutafanya kazi pamoja na mtambue pesa yenu iko salama," alisema Bashe.

Alisema NSSF ni mdau mkubwa katika sekta ya kilimo, na wameongea nao na kuangalia njia bora ya kuwekeza kwenye sekta hiyo kwenye miradi mingine ambayo ipo chini ya Wizara ya Kilimo.

Katika hatua nyingine Bashe alisema kuanzia sasa, taasisi yoyote iliyo chini ya Wizara ya Kilimo, itakayokopa fedha katika taasisi kama NSSF ni lazima wafanyakazi wa kiwanda wawe wanachama wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, kwa kuwa NSSF ndio iliyotumika kutoa mkopo na kwamba ni vyema wanufaike na mkopo huo kwa kuwa moja ya lengo la NSSF ni wafanyakazi wa viwandani waweze kuwa wanachama wa NSSF.

Naye Waziri Mhagama, aliitaka CPB kufanya mazungumzo ya mara kwa mara na NSSF ili kuleta ufanisi zaidi na kutatua matatizo yaliyopo pamoja.

Aliwahakikishia wanachama na wadau kutambua kwamba NSSF ipo imara na kazi ya kukusanya michango iko vizuri.

"Mwaka 2020 nimefarijika sana, kwani kwa mwaka 2017/2018 NSSF kwa mwezi ilikuwa inakusanya wastani wa Sh. bilioni 55 kwa mwezi, lakini mwezi Desemba 2020 makusanyo yamefika Sh. bilioni 111.37 kwa mwezi, ambapo ni mara ya kwanza shirika hilo kufikia kiasi hicho cha makusanyo ya michango kwa mwezi. Makusanyo hayo yataleta tija endapo yatawekezwa katika maeneo sahihi ili baadaye shirika liweze kulipa mafao ya wanachama kwa wakati; ambapo hadi sasa thamani ya shirika imeendelea kuongezeka na kufikia kiasi cha shilingi trilioni 4.8 mwaka 2020 kutoka kiasi cha Sh. trilioni 3.1 mwaka 2018.

# TMA yatahadharisha mvua kubwa, upepo mikoa minane

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imetoa tahadhari ya kuwapo kwa mvua na upepo mkali katika baadhi ya maeneo katika mikoa minane kwa siku nne mfululizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na mamlaka hiyo kwamba kutakuwapo na hali mbaya ya hewa kuanzia Januari 10 hadi 13, mwaka huu, hivyo kutoa tahadhari kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo.

TMA ilibainisha mikoa ya Mbeya, Songwe, Iringa, Njombe, Ruvuma, Lindi, Mtwara, pamoja na Kusini mwa Mkoa wa Morogoro, itakumbwa na mvua kubwa kwa kipindi hicho.

Kadhalika, baadhi ya maeneo ya Pwani ya Bahari ya Hindi ikihusisha mikoa ya Tanga, Dar es Salaam, Pwani, visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba vitakumbwa na upepo mkali utakaovuma kwa kilometa 40 kwa saa.

Taarifa hiyo ilieleza: "Angalizo la upepo mkali unaofikia kilometa 40 kwa saa, mawimbi makubwa yanayofikia mita mbili itaikumba mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani ikijumuisha visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba."

Kadhalika ilieleza kuwa: "Wastani wa athari zinazoweza kujitokeza ni baadhi ya makazi kuzungukwa na maji, pamoja na ucheleweshwaji wa shughuli za uvuvi na usafirishaji."

Kadhalika, TMA iliwaomba wananchi wanaoishi katika mikoa hiyo kuendelea kufuatilia taarifa zitakazoendelea kutolewa na kuchukua tahadhari.


bam

## BAM International JNIA T3 equipment & vehicle sales

| | Vehicles, trucks & trailers | Capacity | YoM | Hrs/kms | Registration | USD all incl. | TZS all inclusive |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Toyota Fortuner 3.0D4D 4WD, A/T | 135hp | 2016 | 141,164 | T 517 DGS | 26,500.00 | 61,745,000 |
| 2 | Ford Ranger 3.2Tdi XL 4WD DC pickup, A/T | 200hp | 2014 | 96,141 | T 491 DCQ | 21,500.00 | 50,095,000 |
| 3 | Ford Ranger 3.2Tdi XL 4WD DC pickup, A/T | 200hp | 2014 | 80,860 | T 526 DCQ | 21,500.00 | 50,095,000 |
| 4 | Ford Ranger 3.2Tdi XL 4WD DC pickup, A/T | 200hp | 2014 | 82,531 | T 525 DCQ | 21,500.00 | 50,095,000 |
| 5 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 60,089 | T 502 DCQ | 6,500.00 | 15,145,000 |
| 6 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 42,670 | T 522 DCQ | 6,800.00 | 15,844,000 |
| 7 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 76,290 | T 498 DCQ | 6,500.00 | 15,145,000 |
| 8 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 100,922 | T 500 DCQ | 6,500.00 | 15,145,000 |
| 9 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 67,429 | T 515 DCQ | 6,500.00 | 15,145,000 |
| 10 | Ford EcoSport 1.5L Titanium - De-registered | 110hp | 2014 | - | - | 1,050.00 | 2,446,500 |
| 11 | Ford EcoSport 1.5L Ti-VCT Trend, A/T | 110hp | 2014 | 81,470 | T 530 DCQ | 6,500.00 | 15,145,000 |
| | Construction equipment | Capacity | YoM | Hrs/km | Licence no. | USD all incl. | TZS |
| 12 | **Terex RT75 mobile rough terrain crane** | 75 tons | 2014 | 9,121 | T817DBY | 324,500.00 | 756,085,000 |
| 13 | Nissan UB01 electric forklift 1.5t | 1.5t | 1996 | - | | 5,050.00 | 11,766,500 |
| 14 | Telschig KB-320-E cement transfer blower | 320m3\min | 2007 | N/A | | 2,250.00 | 5,242,500 |
| 15 | Bema hydraulic road sweeper 2.25m attachm. | 2.25m | 2010 | N/A | | 1,050.00 | 2,446,500 |
| 16 | Cat 428-432 backhoe 5 in 1 bucket | 800ltr | 2014 | N/A | | 1,250.00 | 2,912,500 |
| 17 | Hüdig - Deutz HC532/07 water pump | 270 M3/hr | 2012 | - | | 4,500.00 | 10,485,000 |
| 18 | **Intrame UM-260 asphalt plant** | 260 ton/hr | 2012 | 300,000ton | | 324,500.00 | 756,085,000 |

**The above given information is to our best knowledge, no rights can be derived from the given information.**

**The list prices are inclusive of duties (where applicable) and VAT and are sold under the condition of: "as is, where is".**

In addition to the above mentioned vehicles and equipment we have for sale left overs from the recent auction such as;

Floor grinding and polishing machines (Terrazzo) and consumables for same, industrial chillers and air conditioners, air ducts and louvers, plumbing materials and consumables, ceramic floor & wall tiles, ceiling tiles, hand and power tools, concrete production aids; backing rods, spacers, expansion joints. HDPE & PVC connectors, fittings & piping, cementitious boards, insulation materials, exit doors, fire fighting installation materials and ancillaries, Hilti hardware, general hardware, 8mm threaded bars 3.0m, general building consumables etc. etc.

**For further information or inspection please visit our yard at the below address or call; 0769 445319 for Swahili and English or 0745 555660 for English only.**

**BAM International bv - Africa, Project site yard at Airport Road (Jet Lumo), Dar es Salaam**

## DC aagiza meneja kampuni madini kuwekwa mahabusu

**Happy Severine, BARIADI**

MKUU wa Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, Festo Kiswaga, ameagiza kukamatwa na kuwekwa mahabusu Meneja wa Kampuni ya Madini ya EMJ, Juvenari Mrashani, kwa madai ya kukaidi maagizo ya serikali.

Kampuni hiyo ambayo ilipewa kibali cha kusimamia mgodi wa dhahabu wa Lubaga ulioko Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, mkoani Simiyu, inadaiwa kukaidi agizo la serikali la kulipa ushuru wa mifuko ya 1,000 mawe ya dhahabu, pamoja na mrabaha wa serikali.

Kabla ya kufika uamuzi huo, Kiswaga alimtaka meneja huyo kueleza sababu za kushindwa kulipa ushuru wa serikali pamoja na mrabaha.

Hata hivyo, meneja huyo alishindwa kujibu swali hilo na kudai hafahamu lolote juu ya deni hilo.

"Kampuni hii imekuwa na usumbufu mkubwa, mmekuwa mkikaidi maagizo ya serikali, mmekaidi maagizo ya Mkuu wa Mkoa, Waziri wa Madini, leo ni zaidi ya wiki tatu mmegoma kulipa ushuru wa mawe hayo na mrabaha zaidi ya Shilingi milioni nane," alisema Kiswaga na kuongeza:

"Leo nitaondoka na wewe meneja, utawekwa ndani mpaka pale mtakapolipa, Polisi kamateni huyu meneja, asitoke mpaka walipe ushuru na mrabaha, hatuwezi kuwa na watu wanatuchezea, wamejifanya wao wako juu ya sheria," alisema Kiswaga.

Baada ya kukamatwa meneja huyo, Kiswaga aliongea na wanunuzi wadogo wa dhahabu katika mgodi huo na kutoa agizo kuwa hakutakuwa na msamaha kwa mtu yeyote atakayematwa anatorosha madini.

"Juzi tumemkamata mmoja, tukampiga faini na mawe tukataifisha, kuanzia sasa hatutafanya hivyo, ukikamatwa moja kwa moja mahakamani unakutaka na uhujumu uchumi, hatutakuwa na mzaha, hivyo epukeni hilo."

# Mwalimu mbaroni madai kumbaka mwanafunzi ofisini

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Namibu B, katika Halmashauri ya Bunda mkoa wa Mara (jina tunalo), anashikiliwa na polisi wilayani humo kwa madai ya kumbaka mwanafunzi wa darasa la sita.

Polisi Bunda imethibitisha tuhuma hizo na kueleza kuwa alibakwa asubuhi katika ofisi ya mwalimu mkuu wa shule hiyo baada ya kuzibwa mdomo na kutishiwa kuuawa.

Hata hivyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mara, Daniel Shilla, alipoulizwa kuhusu madai hayo, alisema hana habari za kutokea tukio hilo na kuahidi kufuatilia na kutoa taarifa.

Kwa upande wa Polisi Bunda, ulidai kuwa mwanafunzi huyo siku ya tukio alikuwa akitoka kumsindikiza mama yake mzazi aliyekuwa anasafiri na kwamba alipopita eneo la shule mwalimu huyo alimuita na kumuamuru aingie ofisini kwake.

Ilidaiwa kuwa alipoingia ofisini mwalimu huyo alifunga mlango na kumbaka akimziba mdomo kumtishia kuwa akithubutu kumwambia mtu yeyote atamuua.

Baada ya kufanyiwa ukatili huo mwanafunzi huyo mwenye umri wa miaka sita alikwenda nyumbani kwao na kuwaleza ndugu zake.

Baada ya taarifa kujulikana mwalimu huyo alikamatwa na polisi wa kituo kidogo cha Kibara na kupelekwa kituo kikuu cha wilaya mjini Bunda.

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo (jina tunalo), alisema siku hiyo akiwa safarini alipigiwa simu kuhusu tukio hilo na akaamua kuahirisha safari yake na kurudi ili kutoa taarifa polisi.

Alisema, baada ya mwalimu kukamatwa cha ajabu alificha jina lake polisi na kuandika jingine na kuiomba serikali kungilia kati ili haki itendeke kwa sababu binti yake amefanyiwa ukatilii huo na atakuwa ameathirka kisaikolojia.

"Naomba sana serikali yangu inayoongozwa na rais mpenda watu Magufuli aingile kati maana tunapeleka watoto shuleni tena kwa gharama za serikali siyo kwenda kunyanyaswa na walimu, naomba iingilie kati ili haki itendeke," alisema mama huyo.

Polisi mmoja wa kituo kidogo cha polisi Kibara ambaye hakutaka kutaja majina yake kwa maelezo kuwa siyo msemaji wa jeshi hilo, alidai kuwa mwanafunzi huyo alipelekwa katika hospitali ya misheni Kibara na kufanyiwa uchuguzi.

Kwa upande wake mwanafunzi aliyefanyiwa unyama huo, akizungumza na gazeti hili alisema kuwa alipoitwa na mwalimu baada ya kumsindikiza mama yake, alimtii bila kufahamu kitakachomtokea.

Alisema kuwa mara kwa mara mwalimu huyo amekuwa akimwambia kwamba anapendeza sana.

"Nilikuwa nikishangaa sana mwalimu wangu kunitamkia maneno hayo," alisema.



Baadhi ya wanachama wa CHADEMA, Jimbo la Makambako, mkoani Njombe, wakisomba matofali kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya jimbo ya chama chao, juzi.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wakulima wapewa mbegu za mahindi bure

**Na Neema Hussein,** RUVUMA

KATIKA jitihada za kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji na kukuza vipato vyao, Mkoa wa Ruvuma umewapatia wakulima zaidi ya 4,000 kutoka vijiji vya Halmashauri ya Mbinga mbegu bora za mahindi za kupanda msimu huu.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa mbegu hizo, Kaimu Ofisa Kilimo wa Halmashauri, Deodatus Kisima, alisema mchakato wa mpango huo umetokana na maombi ya uhitaji wa mbegu kutoka serikali kuu kupitia serikali ya mkoa ambao awali walikubaliwa kuwapata tani nne.

Kwa mujibu wa Kisima, kutokana na mahitaji makubwa ya mbegu kwa wakulima katika halmashauri hiyo, serikali iliona ni vyema kuwaongezea hadi kufikia tani nane, hata hivyo katika hatua ya mwisho ya utekelezaji halmashauri ilipata tani 11 ambazo ni sawa na kilo 11,000 za mbegu ya mahindi zenye thamani ya Sh. milioni 77.

Kisima alisema, katika mpango huo kila mkulima atapata kilo mbili hadi nne za mahindi DK 90-89 ambazo zinafaa kwa mazingira ya eneo hilo na kueleza kuwa uteuzi wa wakulima ulifanywa na maofisa watendaji wa maeneo yaliyolengwa kupata mbegu kwa ajili ya kilimo cha mahindi.

Maeneo yaliyolengwa na kupatiwa mbegu hizi ni vijiji vya kata ya Amani, Makolo, Mkako, Namswea, Muungano, Matiri, Muhongozi, Kitumbalomo, Kigonsera, Kihangimahuka na Lukarasi.

Alisema, katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi, halmashauri imeorodhesha na kupata wakulima ambao wamenufaika na mpango na wataalam wa kilimo kutoka maeneo hayo wameelekezwa namna ya kusimamia.

Kisima, ameishukuru serikali kwa kufanikisha upatikanaji wa mbegu ambazo zitasaidia kuongeza uzalishaji katika ngazi ya kaya, halmashauri, mkoa na taifa.

Akizindua mpango huo na kukabidhi mbegu kwa wakulima, Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya, Samwel Komba, aliwataka wakulima waliopata mbegu hizo kuzitumia kikamilifu na kushirikiana na wataalam wa kilimo ili kuvuna mavuno mengi.

Aliwataka maofisa kilimo na watendaji wa vijiji kuhakikisha mbegu hizo zinawafikia walengwa katika maeneo husika na kuepuka kugawana kwa kujuana.

Alisema, mbegu hizo zimetolewa kwa wakulima kama fidia ya janga la corona na lengo ni kuongeza uzalishaji kwa wakulima wa halmashauri na kuishukuru serikali kwa msaada.

Aliwataka wasimamizi wa mpango huo kufikisha mbegu hizo kwa walengwa na kuhakikisha wanazingatia maelekezo yaliyotolewa na serikali.

HABARI KITAIFA

# Kipanga awasimamisha kazi maofisa wanne VETA

**Na Futuna Suleiman**

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga, amewasimamisha kazi maofisa wanne wa Chuo cha Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Mkoa wa Lindi.

Kipanga amefikia uamuzi huo wakati alipokuwa akikagua mradi wa ujenzi wa Chuo cha VETA cha Wilaya ya Mafia ambacho ujenzi wake unasimamiwa na chuo hicho Lindi.

Alisema amechukua hatua hiyo baada ya kugundua ukiukwaji mkubwa wa taratibu katika kutunuku zabuni ikiwamo kumtunuku mwalimu wa Chuo cha VETA Lindi, Rose Mlelwa na mafundi kufanya kazi bila ya mikataba.

Watumishi hao waliosimamishwa ni Mkuu wa Chuo, Ofisa Ugavi na Ununuzi, Mhasibu na Mkaguzi wa Ndani, Kipanga ameagiza Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mafia na Lindi kuwachunguza iwapo hawakuwa na maslahi binafsi katika kusimamia ujenzi wa mradi huo.

"Kuanzia leo nawasimamisha kazi Mkuu wa chuo VETA Lindi, Ofisa Ununuzi, Daniel Solomon, Mhasibu na Mkaguzi wa Ndani, Richard Peter, ili kupisha uchunguzi na nawaagiza TAKUKURU Mafia mshirikiane na Lindi kuwachunguza hawa ili tujue kama hawakuwa na maslahi binafsi kwenye mradi huu," alisema Naibu Waziri Kipanga.

Pia, aliwasimamisha mafundi wote waliopewa kazi ya ujenzi wa majengo zaidi ya moja na kuwataka kila mmoja ajenge jengo moja pekee kama utaratibu unavyotaka, kutokana na mafundi hao kutokuwa na nguvukazi ya kutosha kukamilisha ujenzi kwa wakati na kuwataka wanaosimamia mradi kuhakikisha wanapatikana mafundi wengine haraka ili kukamilisha ujenzi huo.

"Nataka mafundi wote waliopewa kazi ya kujenga zaidi ya jengo moja wabakie na ujenzi wa jengo moja tu sababu hawana uwezo wa kutosha kukamilisha ujenzi kwa wakati na hivyo watasababisha kuzidi kuchelewa," alisisitiza Kipanga.

Awali, akisoma taarifa ya ujenzi kwa niaba ya Mkuu wa Chuo cha VETA Lindi, Richard Shekidele, alisema kuwa mpaka sasa Sh. bilioni 1.1 zimeshapokelewa kwa ajili ya mradi huo na umefikia asilimia 31.5.

Serikali inajenga jumla ya vyuo ya VETA 25 katika wilaya mbalimbali nchini vitakavyogharimu Sh. bilioni 1.6 kila kimoja.

# NHC yawatangazia kiama wadaiwa sugu

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC), limetangaza kuanza kuwachukulia hatua wapangaji wadaiwa sugu ikiwamo kuwaondoa kwenye nyumba, kukamata mali zao na kuzinadi, ifikapo mwishoni mwa mwezi huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na NHC, inadai zaidi ya Sh. bilioni 27 ikiwa ni malimbikizo ya upangishaji nyumba zake.

Shirika hilo lina wapangaji 17,000 katika mikoa mbalimbali nchini zikiwamo taasisi za umma na binafsi wanaodaiwa kodi kama malimbikizo baada ya kushindwa kulipa kwa wakati.

Akizungumza wakati wa kikao cha Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula na watendaji wa sekta ya ardhi jijini Arusha, Meneja Huduma za Jamii na Uhusiano wa NHC, Muungano Saguya, alisema kwa jiji la Arusha pekee shirika lake linadai wapangaji zaidi ya milioni 370 na kusisitiza kuwa zoezi hilo ni la nchi nzima.

Alisema, njia pekee kwa wadaiwa wa kodi ya pango la nyumba wa shirika hilo kuepuka kuchukuliwa hatua ikiwamo kuwatangaza katika vyombo vya habari ni kuhakikisha wanalipa malimbikizo na kodi wanazodaiwa kabla ya Januari 31, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Saguya, NHC linategemea fedha za wapangaji wake na miradi mbalimbali inayofanya kujiendesha, kutolipwa fedha za upangishaji ni kufifisha juhudi zake kujiendesha kibiashara.

Saguya alisema: "Shirika letu la NHC linategemea fedha za upangishaji nyumba zake na miradi kujiendesha kibiashara, hivyo kutolipa kodi kunalifanya shirika kushindwa kujiendesha kwa ufanisi."

Kwa upande wake Naibu Waziri, Dk. Mabula alisema kazi inayoendelea ya kuwafikisha wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya wilaya iende sambamba na kuwachukulia hatua wapangaji wanaodaiwa kodi ya nyumba.

Alisema, NHC inategemea kwa asilimia mia kujiendesha, wapangaji kushindwa kulipa kodi kwa wakati kunalifanya kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

"Msako wa kodi ya ardhi na pango la ardhi uende sambamba pia na wale wadaiwa wa Shirika la Nyumba la Taifa maana shirika hujitegemea kwa asilimia mia, tusipolipa tutalikwamisha kufanya kazi," alisema Dk. Mabula.

# Mtoto afariki dunia kwa kutumbukia kwenye dimbwi

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

MTOTO Isack Joseph (1), mkazi wa Mtaa wa Bupandagila, Halmashauri ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu, amefariki dunia baada ya kutumbukia kwenye dimbwi la maji jirani na nyumbani kwao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa huo, Magesa Makingi, alisema tukio hilo lilitokea juzi baada ya mtoto huyo kuwatoroka watoto wenzake na kuelekea kwenye dimbwi hilo huku wazazi wake wakiwa shambani.

Alisema taarifa za tukio hilo walizipata kutoka kwa baadhi ya watu waliokwenda katika dimbwi hilo ili kuchota maji.

Baba mkubwa wa mtoto huyo, Yohana Makali, alisema kifo cha mtoto wao hakihusishwi na mtu yeyote na kwamba dimbwi hilo linatumika kuchota maji kwa matumizi ya familia kama kufua na kuoshea vyombo.

"Tumepokea kwa masikitiko makubwa kifo cha mtoto wetu na hakuna wa kulaumiwa cha msingi ni kuongeza umakini katika kuwalinda watoto dhidi ya mazingira hatarishi," alisema Yohana.


**MNADA WA HADHARA WA NYUMBA**

NYUMBA ILIYOPO MTAA WA **AMANI** KATA YA **LIWITI ILALA DAR ES SALAAM** INAYOMILIKIWA NA **KISSA P.KYETO**. MHUSIKA WA MNADA NI **J&J REOVERIES, MDAI NI HARBOR MICROFINANCE CO.LTD.** TAREHE YA MNADA NI **11/01/2021 SAA3 ASUBUHI** NA KUENDELEA KWA MAWASILIANO NAMBA **0714 292260/0718802350**

**MASHARTI YA MNADA**

1. 25% italipwa siku ya mnada na 75% ndani ya siku 14
2. Dhamna itauzwa kama ilivyo na gharama za kuhamisha umiliki ni za mnunuzi mwenyewe.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA FORM II
(S.M.M 1984 NYONGEZA)
YA KANUNI YA 2.

Katika mahakama ya mwanzo **BUGURUNI**

Usimamizi wa mirathi **06/2021**

Ombi la **OMARI MOHAMED MANJONJO** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **HASSAN MOHAMED MANJONJO**

kwa watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **04/02/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hio.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.


**TENDER**

**FOR HIRING SCHOOL BUS**

HBS Hannah Bennie Schools

**NO.5 Mkoa wa DSM**

**Matokeo ya NECTA STD 4, 2019...**

***Sasa inafanya usajili wa Nursery na Primary.***

**0620 301 010 / 0762 224 224**




Hannah Bennie Schools "HBS" a private school in kibugumo, kigamboni is looking for reputable, experienced and financially sound company/ partnership firm/agency to provide vehicles (school buses) in excellent condition on lease basis.

Details of the tender can be obtained from our website **www.hbs.ac.tz** or **Instagram page @hbs.tanzania**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Simba, Namungo zikijipanga mapema inawezekana Caf*

**TAYARI** Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), limeweka wazi ratiba yake ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa na mechi za mchujo za Kombe la Shirikisho, ambapo kwa Tanzania Bara inawakilishwa na Simba na Namungo FC.

Simba ambayo inapeperusha bendera ya Tanzania kwa upande wa Ligi ya Mabingwa yenyewe ipo Kundi A pamoja na Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan.

Na kwa upande wa Namungo inayoipeperusha bendera ya nchini kwenye Kombe la Shirikisho, imetinga hatua ya mwisho ya mechi za mchujo na ratiba ikionyesha itaanzia ugenini Februari 14, mwaka huu dhidi ya Clube Desportivo 1º de Agosto ya Angola na kama itapata matokeo ya jumla kwa mechi mbili ya ugenini na nyumbani, itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Lakini kwa Simba ambayo nayo Februari 12, mwaka huu itaanzia ugenini dhidi ya AS Vita, yenyewe inachotakiwa ni kuhakikisha inamaliza nafasi ya kwanza ama ya pili katika kundi lake ili kukata tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Kwa kiwango ambacho Simba na Namungo zimeonyesha hadi sasa kwenye michuano hiyo, tunaamini zikiendelea kujipanga kwa kufanyia kazi kasoro ndogondogo zilizojitokeza, zinaweza kufika mbali katika michuano hiyo.

Namungo ambayo ilifika hatua hiyo kwa kuitoa Al-Rabita ya Sudan Kusini kwa jumla ya mabao 3-0 kwenye raundi ya awali kisha raundi ya kwanza ikaitupa nje Al Hilal Obayed ya Sudan kwa jumla ya mabao 5-3, tunaamini mechi hizo mbili zimeipa uzoefu mkubwa katika mashindano hayo ambayo inashiriki kwa mara ya kwanza, lakini pia zimeiwezesha kujua wapi pakujiimarisha zaidi.

Aidha, kwa Simba ambayo imetinga hatua ya makundi kwa kuitoa Plateau United ya Nigeria kwa bao 1-0 kwenye raundi ya kwanza kabla ya kuifurusha nje FC Platinum ya Zimbabwe kwa jumla ya mabao 4-1, hatuna wasiwasi nayo kwa upande wa uzoefu kwenye michuano ya kimataifa.

Lakini inapaswa kujiimarisha vema katika safu yake ya kiungo na ulinzi, huku ikikamilisha mapema mchakato wa kocha mkuu mpya wa kuziba pengo la Sven Vandenbroeck ambaye ameachia ngazi baada ya kuiwezesha timu hiyo kufuzu hatua ya makundi.


Tunatambua Sven tayari alishawajua vema wachezaji wake na namna ya kuwatumia, hivyo kocha mpya ni muhimu kupatikana mapema ili kuwazoea wachezaji lakini nao wapate muda wa kuzifahamu falsafa zake na mfumo atakaoutumia.

Tunaamini huu ni msimu sahihi kwa Simba na Namungo kuweza kuutumia vema kwenye michuano hiyo ili kufika mbali hasa kutokana na timu nyingi kutokuwa mashindanoni kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona tofauti na Tanzania ambapo ligi na michuano mbalimbali imekuwa ikiendelea.

Simba na Namungo ambazo kwa sasa zipo kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi visiwani Zanzibar, tayari zimecheza mechi za Kombe la FA pamoja na Ligi Kuu inayoshirikisha timu 18, ambayo kwa sasa inaingia mzunguko wa pili.

Lakini ukitazama kwa wapinzani wao, ni AS Vita pekee ambayo ligi ya kwao DR Congo ipo raundi ya 14, lakini zingine hakuna iliyozidi raundi ya tano, hivyo tunaamini kama Simba na Namungo zitajiimarisha na kujipanga ndani na nje ya uwanja, zinafaidika zaidi kwa wachezaji wao kuwa timamu kimchezo ukilinganisha na wapinzani wao wengi ambao ligi za kwao ndiyo kwanza zimeanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwangwo

# *Magufuli alivyozibeba Simba, Namungo michuano ya CAF*

**NI** ukweli usiopingika kabisa kuwa uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kuruhusu michezo kuendelea wakati nchi zingine zikiwa zimejifungia ndani kutokana na janga la ugonjwa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona, pia umechangia kufanya vema kwa timu za Tanzania, Simba na Namungo kwenye michuano ya kimataifa msimu huu.

Simba imefanikiwa kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuzitoa timu ngumu za Plateau United ya Nigeria kwa bao 1-0 na FC Platinum ya Zimbabwe kwa jumla ya mabao 4-1.

Timu ya Namungo FC ambayo inaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, nayo imetinga raundi ya pili ya michuano hiyo baada ya kuziondoa Al Rabita ya Sudan Kusini kwenye mechi ya awali na kwenye raundi ya kwanza iliichapa Al Hilal Obeid ya Sudan kwa jumla ya mabao 5-3, ikishinda 2-0 nyumbani na kutoka sare ya mabao 3-3 ugenini.

Mei mwaka jana, Rais Magufuli, pamoja na mambo mengine, aliruhusu kuendelea kwa michezo yote, ikiwamo Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa ni nchi pekee kama si chache Afrika kuendelea na ligi.

Kitendo cha kuendelea na michezo kimeonekana kuleta faida kubwa, kwani ushindi wa timu zote za Simba na Namungo, pamoja na mipango ya viongozi na mabenchi ya ufundi, uwezo wa wachezaji, lakini kuna ukweli kuwa timu nyingi bado haziko fiti sana kutokana na nchi zao kukaa muda mrefu bila kucheza soka.

Wakati nchi zingine zikianza kuruhusu soka kuchezwa na Shirikisho la Soka Afrika kuruhusu kuanza kwa michuano ya Ligi ya Mabingwa na Shirikisho, wachezaji wanaocheza Ligi Tanzania imewakuta wako fiti kimwili kutokana na wao waliendelea kucheza, huku wachezaji wa timu nyingi za nje pamoja na uwezo wao, lakini walionekana kukosa utimamu wa mwili kutokana na kukaa muda mrefu na bado hawajaanza kuchanganya.

Timu za Tanzania zinaweza kuendelea kuipata faida hii kwenye mechi zinazofuata, kwani wakati wachezaji wa timu zingine wakianza kuchanganya, tayari wanaocheza soka Tanzania watakuwa mbali sana.

Simba imepangwa Kundi A, ikiwa na timu za AS Vita ya Congo DR, mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri na Al Merreikh ya Sudan.

Imepangwa kwenye kundi lenye timu ambazo ilikuwa nazo mwaka 2019, kasoro JS Saoura ya Algeria ambayo imeipisha Al Merreik. Kuna baadhi ya mashabiki wanaona kama itakuwa ngumu mno kwa Simba kupenya kwenye kundi hilo, lakini kama itakuwa imejizatiti inaweza kutinga hatu ya robo fainali kama ilivyofanya mwaka 2019. Tena inaweza kuwa ni rahisi zaidi kwao kwa sababu safari hii itakuwa inacheza ugenini kukiwa hakuna mashabiki, huku Tanzania yenyewe ikiruhusiwa kuingiza asilimia 30 ya mashabiki uwanjani.

Rais Magufuli aliwaambia wananchi waendelee na shughuli zao, badala yake wamuombe mwenyezi Mungu kuiondoshea nchi ugonjwa huu na kwa kiasi kikubwa imefanikiwa, na imekuwa faida kubwa hata kwenye michezo.

Tumeona Simba ikicheza Nigeria na Zimbabwe viwanja vikiwa na watu wachache sana, na hiyo ikiendelea itakuwa faida kwa wawakilishi hao wa Tanzania na sidhani kama wanaweza kufungwa tena mabao matano ugenini.

Wakati Simba ikicheza raha mustarehe ugenini, hapa nyumbani timu za ugenini zinakutana na mashabiki wanaoruhusiwa kuingia uwanjani, hivyo kuwa na wakati mgumu mno.

Namungo ambayo pia imenufaika na hilo, nayo pia itapambana na Clube Desportivo 1º de Agosto ya Angola kwenye mechi ambayo kama ikishinda itakuwa imetinga kwenye hatua ya makundi ya shirikisho.

Wawakilishi wa Tanzania, Simba na Namungo, zinaweza kuishangaza Afrika mwaka huu kwa kufika mbali kwenye michuano hiyo, mbali na sababu za kiufundi, lakini uamuzi wa Rais Magufuli kuruhusu michezo kuendelea, lakini mashabiki kuruhusiwa viwanjani kuzishangilia timu hizo, wakati kwao kwa sasa hakuna vitu kama hivyo, na kuzifanya mechi zao za nyumbani zisiwe tishio sana kwa timu za Tanzania.

# Wanamwambao Tanganyika waonyeshwa fursa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, amewataka wanaoishi kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika, kutumia miundombinu ya kisasa ya bandari na barabara, kuwekeza miradi ya kiuchumi na kuboresha maisha yao.

Aliwaambia wakazi wa mikoa ya Songwe, Rukwa, Katavi na Kigoma kutumia fursa za ujenzi wa barabara na bandari za kwenye Ziwa Tanganyika ili kukuza uchumi wa maeneo yao.

Taarifa ya Kitengo cha Mawasiliano serikalini, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, ilisema hayo jana alipokagua maendeleo ya ujenzi wa barabara za Mpanda hadi Vikonge yenye kilometa 35 na ya Kasinde hadi Mpanda yenye kilometa 105.389.

Alisema alikagua pia yenye kilometa 112 inayoanzia Kagwira hadi Karema na Bandari ya Karema iliyoko mkoani Katavi ambayo ujenzi wake unaendelea.

Akizungumzia fursa hizo, alisema ni pamoja na kupata ajira kwa wenye taaluma, kuzalisha mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na biashara katika mwambao wa ziwa Tanganyika ambao umeanza kuvutia wawekezaji wengi katika siku za hivi karibuni.

Alizitaja bandari nyingine zinazojengwa katika ukanda wa Ziwa Tanganyika kuwa ni Kabwe na Kasanga ambazo zote zitakapokamilika zitaongeza huduma za usafiri na uchukuzi katika ziwa hilo na nchi jirani, hivyo kukuza biashara katika mwambao huo.

Aidha, alimtaka Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS), Mkoa wa Katavi, kuhakikisha barabara ya Kagwira hadi Karema inayounganisha mji wa Mpanda na Bandari ya Karema inapitika wakati wote.

Alisema nia ni kuharakisha ujenzi wa bandari hiyo na hivyo kuwezesha wawekezaji kufika kwa urahisi katika eneo hilo ili kuona fursa za kiuchumi na kijamii.

Meneja wa TANROAD Mkoa wa Katavi, Martin Mwakabende, alimweleza Naibu Waziri kuwa Sh. bilioni 1.2 zimetengwa kwa ajili ya kuiboresha barabara hiyo kipindi hiki cha mvua nyingi wakati mchakato wa kuijenga kwa kiwango cha lami ukiendelea.

Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Salehe Mhando, alisema wilaya itashirikiana na makandarasi wote wanaosimamia miradi katika eneo hilo ikiwamo ulinzi na watumishi wenye sifa ili kukamilisha miradi ya ujenzi kwa wakati.

Bandari ya Karema ambayo inatarajiwa kuwa kubwa katika ukanda wa Ziwa Tanganyika inajengwa na mkandarasi kutoka China na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Kukamilika kwa bandari hiyo, kutachochea biashara kati ya Tanzania na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Burundi na kukuza uchumi katika mikoa ya ukanda wa magharibi.

SOS CHILDREN'S VILLAGES ZANZIBAR

# JOB OPPORTUNITIES

SOS Children's Villages Zanzibar is Local Non- Government Organization (NGO) affiliated to SOS Children's Villages International, a worldwide child care organization that work to protect and care for children who have lost parental care, or who stand at risk of losing it. Established 64 years ago, SOS Children's Villages International currently has Children's Villages and other projects in 135 countries around the world. Globally, it runs two major programmes i.e. Family Based Care based at SOS Children's Villages and Family Strengthening Programmes supporting families in local communities. SOS has been working in the United Republic of Tanzania since 1991, and runs Children's Villages and other projects in Tanzania, the organisation runs four Children's Villages in Arusha, Dar es Salaam, Mwanza and Zanzibar and other programmes in Pemba, Iringa and Mufindi.

**Job title: Assistant Accountant /Data Entry Clerk (1 post)**
**Duty station: SOS Children's Village Zanzibar**
**Reporting to: Senior Accountancy & Alternative Care Coordinator**

The Data clerk receives, reviews, and enters data into computer system or tracking database according to established procedures. He/she is responsible for ensuring accuracy of all data recorded and performs database maintenance functions.

Roles & Responsibilities

- Keeps track of received data and source documents.
- Prepares and sorts source documents, and identifies and interprets data to be entered.
- Contacts prepares of source documents to resolve questions, inconsistencies, or missing data.
- Confirms accuracy of data such as canter name/location, days and dates.
- Compares data entered with sources documents.
- Reviews and makes necessary corrections to data entered.
- Complies, sorts, and verifies accuracy of data to be entered.
- Reviews various data collection forms and suggest improvements if needed.
- Assists in establishing and maintaining an effective and efficient record management system.
- Generates reports and responds to inquiries regarding entered data as requested.

**Knowledge, skills and abilities required**

- Holder of Advance diploma in Accounting and Finance or statistics
- Diploma in IT, Records Management, or related field from a recognized institution.
- Three years of experience in NGO.
- Fluency in English (both written and spoken).
- Good knowledge of Microsoft Office applications (Excel, Word, Outlook).
- Analytical approach to work and professionalism.
- Ability to quickly understand the connections between working processes, to gain an overview of essential points and to simplify (not to complicate) working procedures.
- Ability to work effectively in a multi-site organization with a matrix structure and a geographically-dispersed team.

**Job title: Program Officer (1 post)**
**Duty station: SOS Children's Village Zanzibar**
**Reporting to: Program Coordinator**

**Roles & Responsibilities**

- Lead the implementation of the project as per annual plan
- Facilitate and support the timely programme plans from the approved annual plans and budgets.
- Facilitate the formation and development of Community Task Force to spearhead the programme;
- Facilitate the identification of the beneficiaries of the program
- Support communities in the assessment of root causes leading to child abandonment at family and community levels through use of appropriate participatory tools.
- Conduct the capacity building to the beneficiaries of the program
- Facilitate families' access to essential services required to fulfill their children's developmental needs and rights such as education, nutrition, health care and vital registration.
- Facilitate Capacity building of families as well as the community.
- Facilitate the empowerment of community facilitators in Family Development Planning for their effective and efficient contribution in the strengthening of families.
- Facilitate and support the initial Community Based Organisation capacity assessment in order to come up with the CBO Development Plan.
- Facilitate the developing of the CBO's organizational management capacity, that is, formation of properly constituted boards & committees, writing CBO constitution, legal registration of CBO, developing the CBO vision statement, mission statement, strategy and values.
- Support the CBO capacity building of systems in Financial and accounting policies, procurement policies and procedures, resource mobilization strategies, human resource management policies, project reporting procedures and strategic plans.
- Facilitate regular data collection through appropriate monitoring tools on programme interventions.
- Facilitate stakeholder analysis within the programme, maintaining and updating stakeholders' profiles.
- Facilitate participatory monitoring and evaluation of the programme interventions.
- Keep up-to-date information regarding beneficiaries and services provided
- Conduct regular field visit to the area of the program intervention
- Prepare reports to be shared to different levels within and outside the organization

**Knowledge, Skills and abilities**

- Bachelor degree in Social Work, Community Development, Sociology; Development studies and any relevant field from recognized institutions.
- At least three years working experience preferably with NGO/ INGO in this field.
- Basic facilitation skills.
- Basic Knowledge of Gender, Child rights and Advocacy.
- Ability to work with minimum supervision.
- Computer skills especially Microsoft word, Excel & the Internet.
- A good command of both oral & written English

**Job Title: Driver (2 posts)**
**Duty station: SOS Children's Village Zanzibar (Unguja and Pemba)**
**Reporting to: HR cum Admin Officer**

**MAJOR RESPONSIBILITIES**

- Fulfills the Transport Needs for SOS Children's Villages program per specific area of project
- Ensures the Safety of the car, staff and their properties
- Maintains the Safety and Security of the Vehicles
- Advises the Administrators on technical issues of the cars
- Conducts trips using the shortest possible route. Avoids unnecessary deviations and multiple trips to minimize mileage and time wastage.

**QUALIFICATIONS & SKILLS**

- CSEE and Certificate from any recognized VETA colleges / institutions
- At least two years working experience preferably NGOs
- Basic knowledge on Child rights and child protection
- Ability to work with minimum supervision.
- Must possess VIP driving Certificate
- Fluent in English and Swahili

To apply for this position, send your application letter describing how your experience, qualifications and competencies making you the right candidate for this position, Enclose a detailed updated CV, telephone contacts and details of at least 3 referees with their emails, address & phone numbers. All candidates will be subject to child protection recruitment procedures and checks. Only shortlisted candidate will be contacted. The advert is open from 11th January 2021 to 17th January 2021.

The applications should be addressed to: -

**The Program Director**
**SOS Children's Villages Zanzibar**
**P. O. Box 1923 Zanzibar, Tanzania**
**Or sent by email to**
**Email: recruit.sostanzania@sos-tanzania.org**

**Note: The email subject should indicate the title of the position and location (duty station)**

*SOS Children's Villages Zanzibar is an equal opportunity employer. Only short-listed candidates will be contacted.*

**TENDER No. SOSCVZNZ/21/001 FOR**

**PROVISION OF SECURITY SERVICES TO SOS CHILDREN'S VILLAGE ZANZIBAR -UNGUJA & PEMBA**

**TENDER DATE :11.01.2021**

**INVITATION FOR BIDS**

1. SOS Children's Village Zanzibar now invites sealed Tenders from eligible, reputable and competent Tenders for PROVISION OF SECURITY SERVICES TO SOS CHILDREN'S VILLAGE ZANZIBAR -PEMBA & UNGUJA.
2. The organization will use the Open tendering method to identify potential companies to be engaged in the provision of security services.
3. Interested eligible Bidders may obtain further information from and inspect the tendering documents at the office of Program Director, P.O BOX 1923 Zanzibar from 09:00 am to 4:00 pm on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.
1. A complete set of Bidding Documents in English may be obtained from SOS Children's Village Zanzibar Office upon payment of a non-refundable fee of Tsh. 50,000, payment shall be made to the SOS Children Village Zanzibar, PBZ Bank account no. 0400143001. Upon payment of the tender fee,bidders are required to submit payment slip and an official letter for document request.

1. All bids in one original document plus one copy properly filled and enclosed in plain envelopes clearly marked Tender no. PROVISION OF SECURITY SERVICES TO SOS CHILDREN'S VILLAGE -PEMBA & UNGUJA must be delivered to address below at or before 22nd January 2021.

Procurement Committee
SOS Children's Village
P.O Box 1923
Zanzibar

Tenders will be closed at 10:00 am local time on 22nd January 2021 and Bids will be opened promptly thereafter in Public, in the presence of Bidders or their representatives who choose to attend.

Late Bids, Portion of Bids, Electronic bids not received, Bids not opened and not read out in public at the bid opening ceremony shall not accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

# Kikwazo upimaji ardhi chatajwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

UPUNGUFU wa watumishi na kukosekana vifaa vya kutosha vya upimaji kwenye Idara ya Ardhi mkoani Lindi, kumetajwa kukwamisha kasi ya utoaji huduma na upimaji viwanja mkoani humo.

Hayo yalielezwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi mkoani humo, Said Kijiji, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji na tatizo lililopo kwenye idara hiyo kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula.

Alitoa ripoti hiyo wakati wa kikao kazi kilichofanyika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi, mwishoni mwa wiki.

Taarifa hiyo ilisema vifaa vya upimaji walivyopokelewa kutoka iliyokuwa Ofisi ya Kanda ya Kusini, Mtwara vilikuwa vimeshaharibika na havikuweza kufanya kazi zilizokusudiwa.

Alisema kutokana na ubovu huo, wamelazimika kuvirudisha wizarani kwa matengenezo, huku akiiomba serikali kuipatia Ofisi ya Ardhi Mkoa wa Lindi vifaa vya upimaji viwanja.

Kamishna huyo alitaja changamoto nyingine kuwa ni kukosa kifaa 'scanner' kwa ajili ya upimaji na idadi ndogo ya watumishi, waliopo kwa sasa kwa mkoa mzima ni 18 wakati hitaji halisi ni 28.

Akizungumza katika kikao hicho kilichojumuisha baadhi ya wadaiwa sugu wa kodi ya ardhi, Naibu Waziri wa Ardhi, Angeline Mabula, aliwataka wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya na manispaa, mkoani hapo wasifanye mzaha kusimamia ukusanyaji mapato ya serikali.

Naibu Waziri Mabula alisema anashangazwa kuona fedha nyingi zaidi ya Sh. bilioni 17.0 hazijakusanywa kutoka kwa watu waliopatiwa maeneo, vikiwamo viwanja kwa ajili ya makazi na uwekezaji wa viwanda na mashamba.

"Fedha zipo tatizo kinachokosekana hapo ni namna ya ufuatiliaji, umekuwa hafifu nawaomba zifuatilieni," Mabula aliagiza.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi, alikiri kuwapo kwa upungufu huo na kuahidi kuyafanyia kazi, ikiwa ni pamoja na kufuatilia madeni mikononi mwa wateja.



Kazi ya ujenzi wa Bandari mpya ya Karema ikiendelea wilayani Tanganyika, mkoani Katavi, kukamilika kwa bandari hiyo kutarahisisha shughuli za kibiashara kati ya Bandari ya Karema – Tanzania na Kalemii nchini Kongo DRC. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijana wa kiume wanaopenda 'kulelewa' waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeonya mienendo mipya ya baadhi ya vijana wa kiume kupenda 'kulelewa' na wanawake wenye uwezo kiuchumi hali inayotishia maisha yao.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alitoa onyo hilo na kuwataka wanaume kujiepusha na tabia zinazochochea maambukizi ya VVU na kuacha kuendekeza starehe wanazoziita 'kula bata'.

Aliwataka kuzingatia masoma na kujiandaa kumudu maisha yao badala ya kuendekeza mambo ya kujidhalilisha.

Kigahe alitoa kauli hiyo jana kwenye mahafali ya 55 ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kampasi ya Dodoma na wanafunzi 989 walimaliza masomo yao katika ngazi mbalimbali.

Alisema lipo tatizo jipya kwa vijana kufadhiliwa kwa namna ya kufedheheshwa na baadhi ya wanawake wasiojiheshimu hasa wenye fedha na kuwaharibia masomo yao.

"Ni muhimu sana pia kwa wanafunzi wa kike kuwaepuka wanaume waliojaa utapeli wa kimapenzi ambao unachangia kupoteza mwelekeo kimasomo na hata kuwatumbukiza katika janga la Ukimwi," alisema Kigahe.

Aliwataka wahitimu hao kutumia elimu waliyoipata kwa kutambua fursa na kuzitumia ipasavyo ili jamii itatue kero zinazoizunguka.

Alikiagiza chuo hicho kuanzisha kozi ya uwekezaji na biashara katika mafuta na gesi kwa kuwa ni jambo kubwa la kibiashara litakalokuwa mhimili mkubwa wa kiuchumi Tanzania ndani ya miaka ijayo.

Kadhalika, alisema walimu wanaofundisha masomo ya biashara shule za sekondari na vyuo vya ualimu ni wachache na uhitaji ni mkubwa na kwamba ushirikiano wa CBE na vyuo vya ualimu utaongeza idadi yao.

Alisisitiza kuwa taasisi za elimu ya juu ikiwamo chuo hicho zinatarajiwa kutoa mawazo yenye ushauri wa kiubunifu serikalini na kukihimiza chuo hicho kufanya hivyo.

"Naitaka CBE kuchukua nafasi yake stahiki katika kuongoza shughuli za utafiti, utoaji ushauri wa kitaaluma na uendeshaji wa elimu na mafunzo katika sekta nzima ya biashara," alisema.

Alihimiza kufanya utafiti makini kuwasaidia Watanzania kupata majawabu ya vikwazo mbalimbali katika uendeshaji na usimamizi wa biashara zao kisasa.

"Serikali itaimarisha uwezo wa wahadhiri ili waendelee kufanya utafiti makini kupitia mafunzo mbalimbali na upatikanaji wa vitendea kazi vya kisasa hatua kwa hatua," alisema.

Alisema kuna haja uongozi wa chuo hicho kutafuta mbinu mbalimbali ili kukabiliana na uchakavu wa miundombinu na kwamba wizara itaendelea kuwasiliana na wadau ili kutatua kero hiyo.

Awali, Mkuu wa chuo hicho, Kampasi ya Dodoma, Prof. Emanuel Mjema, alisema kampasi hiyo kwa kushirikiana na vyuo vya ualimu vilivyopo Dodoma, vimeanzisha mchepuo wa walimu wa masomo ya biashara.

"Tutaanzisha uhusiano wa kitaaluma kati CBE na vyuo vya ualimu Dodoma ili kupanua huduma na kuwafikia wananchi wengi zaidi ili kupata walimu wa elimu ya biashara, kwa kuwa kuna tatizo kubwa la walimu kufundisha masomo hayo kwenye shule za sekondari," alisema Profesa Mjema.

Alibainisha kuwa kuna uhaba wa wahadhiri, waliopo ni 49 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi zaidi ya 2,000 na kuomba kibali cha kuajiri.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uongozi wa CBE, Prof. Esther Ishengoma, aliwataka wahitimu hao kutumia elimu waliyopata kujiajiri ili kutengeneza jamii isiyo ya wategemezi.

# TARURA, WB kujenga barabara vijijini

**Na Saidi Hamdani,** LINDI

MKOA wa Lindi ni miongoni mwa maeneo yatakayoanza kunufaika na utekelezaji wa mradi wa barabara za vijijini unaosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), zinazotumia nguvu za wananchi.

Ujenzi huo utagharimu zaidi ya Sh. bilioni 800, kwa mujibu wa Mratibu wa Miradi ya TARURA, Raymond Kileo, katika mahojiano na Nipashe.

Kileo aliitaja mikoa itakayonufaika na mradi huo kuwa ni Tanga, Geita, Njombe na Lindi na kwa Lindi mradi utatekelezwa Wilaya ya Ruangwa na kwamba uteuzi wa maeneo hayo umetokana na data zilizopo kuhusu sehemu zinazozalisha kwa wingi, lakini hakuna miundombinu kufikisha mazao sokoni.

Alisema mpango huo ni wa serikali unaojulikana kama Mpango wa Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji Jamii pamoja na Ufunguaji wa Fursa za Jamii kiuchumi (RISE).

Kileo alisema tofauti na kazi nyingine zilizozoeleka kwa jamii kuona makatapila yakianza kung'oa miti na kuchonga barabara, RISE italenga ushirikishaji wananchi kuanzia ngazi za awali, kabla ya utekelezaji wake rasmi kwa ushirikiano wa serikali kupitia TARURA na Benki ya Dunia (WB).

"Mradi huu unatarajiwa kuchukua miaka sita ya kuutekeleza na sasa hivi ndiyo upo katika hatua za mwanzo ya maandalizi," alisema Kileo.

Alitaja kipaumbele cha awali kuwa ni kutengeneza ajira, kuwezesha wananchi kiuchumi wa maeneo yanayopitiwa na mradi huo. Alisema watapata fursa ya kuajiriwa katika mradi na makundi maalumu wakiwamo kina mama, watu wenye ulemavu na vikundi vinavyoshughulika na mazingira na masuala ya kijamii vitapewa nafasi.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Ruangwa, Mashaka Nalupi, alisema mradi utahusisha barabara sita zinazounganisha wakulima, wafugaji na wachimba madini hadi kufikia barabara kuu za mikoa, lengo likiwa ni kuharakisha usafirishaji mazao.

Alivitaja vijiji vinavyopitiwa na barabara hizo kuwa ni vinavyozalisha korosho na ufuta kwa wingi na vyenye machimbo kama ya kinywe (graphite), dhahabu na rubi.

Nalupi alisema barabara zitajengwa Ruangwa na kuwa kuna sehemu zitajengwa kwa kiwango cha lami hasa maeneo yenye madini mengi ya graphite.

# TPDC yafanya tathmini athari kimazingira mikoa 5

**Na Anthony Ishengoma,** SHINYANGA

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), linafanya tathmini ya athari za kimazingira katika mikoa mitano ya Tanzania ambayo inaguswa na utafiti wa mafuta unaoendelea katika mikoa hiyo ambayo kwa pamoja iko katika bonde la mto Manonga, Wembele na Ziwa Eyasi.

Kwasasa shirika hilo liko katika Wilaya ya Kishapu, mkoani Shinyanga kukutana na wadau pamoja na wananchi walioko katika vijiji vya eneo la mradi kwa lengo la kutoa elimu ili kujiweka tayari kupokea wataalam watakaofanya tathmini hiyo na kupata ufahamu wa ujenzi wa mikuza baada ya kukamilisha tathmini ya kimazingira.

Akiongea na viongozi wa kata na vijiji ambavyo tathmini hiyo itafanyika katika Wilaya Kishapu, mtaalamu mwelekezi wa mradi huo wa mafuta, Dk. Allan Mzengi, alisema utafiti huo umefikia katika hatua ya kushirikisha wadau kwenye eneo la mradi kwa kuwa ni muhimu kwa viongozi na wananchi kufahamu umuhimu wake.

Alisema TPDC iko katika hatua muhimu ya kufanya tathmini ya kimazingira ili kubaini shughuli za kiuchumi katika maeneo hayo na namna inavyoweza kuathiriwa na shughuli za utafiti na hatimaye kushirikiana na jamii husika kupata muafaka kwa manufaa ya maendeleo ya utafiti wa mafuta.

Mtaalamu wa Jiolojia kutoka Shirika la TPDC, Gaston Kanuti, alisema shirika hilo litakapokamilisha hatua muhimu ya kutathmini shughuli za mazingira itawasilisha ripoti ya matokeo ya utafiti huo katika Baraza la Mazingira (NEMC) ili iweze kujiridhisha na kutoa cheti kitachowezesha TPDC kuendelea na hatua muhimu ya uchorongaji wa Mikuza.

Kanuti aliwataka wananchi watakao kuwa katika eneo la mradi kutokuwa na wasiwasi kwa kuwa baada ya utafiti wa data za mitetemo kukamilika, ardhi itakayokuwa imetumika itarudishwa kwa mwenyewe na ikigundulika eneo husika litachimbwa kisima cha mafuta kama yatapatikana mhusika atalipwa fidia.

Alifafanua kuwa uchorongaji wa njia za mikuza utawezesha watafiti kuweka vilipuzi ardhini kwa lengo la kubaini mitego ya mafuta na vitaweka kama inavyoonyeshwa katika ramani ya eneo la utafiti.

Pamoja na ufafanuzi wa mtaalamu wa jiolojia kutoka TPDC, mtaalam mshauri kutoka Kampuni ya MTL Consulting, Abraham Maeda, aliwaambia viongozi hao wa vijiji kuwa utafiti huo wa athari za kimazingira utaangazia pia masuala ya mambo kale akiyataja kuwa ni maeneo ya makaburi na matambiko kwa kuwa ikitokea maeneo kama hayo yanachangamoto mkuza unaweza kupindishwa kuepuka usumbufu.

# FETA watakiwa kuzalisha wataalamu uvuvi bahari kuu

**Na Mbaraka Kambona,** BAGAMOYO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, ameutaka Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) kuongeza kasi ya kuzalisha wataalamu watakaokuwa na uwezo wa kuendesha meli za uvuvi wa bahari kuu zitakazonunuliwa na serikali ili kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi kupitia uchumi wa bluu.

Gekul alitoa kauli hiyo alipofanya ziara katika ofisi za wakala zilizopo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Alisema mpango wa serikali katika miaka hii mitano chini ya uongozi wa Rais, Dk. John Magufuli ni kununua meli nane zitakazotumika kwenye shughuli za uvuvi wa bahari kuu na kwamba ni muhimu kuongeza kasi ya kutoa wataalamu ambao wataziendesha meli hizo zitakapofika.

Aliongeza kuwa mwishoni mwa mwaka huu meli ya kwanza itakuja na kuwa haitapendeza kama vyombo hivyo vitakuja halafu pasiwapo na vijana watakaohusika na kuviendesha.

"Nchi inawategemea mtoe wataalamu watakaosaidia kuendesha meli hizo zitakazoletwa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu, tunaomba mkatuzalishie wataalamu ambao wataendesha vyombo hivyo," alisema Gekul.

Awali akimkaribisha Naibu Waziri, Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, FETA, Dk. Semvua Mzighani, alisema wameshaingia mkataba wa maridhiano wa viwango vya mafunzo na utoaji vyeti kwa wafanyakazi wa vyombo vya uvuvi wa mwaka 1995 na hiyo itasaidia kutoa vyeti kwa manahodha wa meli, maofisa wa meli, mabaharia na waangalizi wa meli zitakazofanyakazi katika uvuvi wa bahari kuu.

"Huwezi kuajiriwa kule kama hauna cheti cha kukutambulisha, hivyo kupitia maridhiano haya sasa mabahari watapatikana kutoka katika chuo hiki," alisema Dk. Mzighani.

Vile vile, alisema kwa Afrika vyuo vinavyotoa mafunzo kwa wataalamu hao vipo Afrika Kusini na Misri na kuwa ni wakati mzuri sasa kupitia mafunzo yatakayotolewa nchini kuongeza ajira kwa vijana na kupata fedha za kigeni kupitia watu kutoka nchi nyingine watakaokuja kusoma katika chuo hicho.

Dk. Mzighani alisema pamoja na mipango na mikakati mizuri waliyonayo katika kuboresha huduma zao bado wanakabiliana na changamoto kubwa ya gharama za uendeshaji wa vyuo vya uvuvi na kuiomba serikali iwaongezee nguvu ili waweze kutoa wataalamu wazuri watakaokwenda kulisaidia taifa kukuza na kuimarisha uchumi wa bluu.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, akiwapa chakula samaki alipotembelea Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA), kampasi ya Mbegani iliyopo wilayani Bagamoyo, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki. Kulia ni Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu, Dk. Semvua Mzighani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kaya zaidi ya 1,000 zapoteza sifa TASAF

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

UHAKIKI wa kaya za walengwa zilizonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini TASAF awamu ya tatu mkoani Njombe katika kipindi cha kwanza (2015-2020), mwezi Julai 2020 hadi Desemba 2020, jumla ya kaya maskini 1,366 zimepoteza sifa ya kuwa kwenye mpango huo.

Vile vile, kaya 17,475 zimebainika kuwa na sifa ya kuendelea kunufaika huku kaya 1,005 hazikuhudhuria uhakiki kwa sababu mbalimbali.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao cha kamati ya ushauri mkoa RCC, Mratibu wa TASAF Mkoa wa Njombe, Mussa Selemani, alisema kwa upande wa kaya ambazo hazikuhakikiwa zitapewa nafasi ya mwisho kabla ya kutolewa kwenye mpango ikiwa hazitajitokeza tena.

"Changamoto kuu iliyojitokeza wakati wa uhakiki ni baadhi ya wakuu wa kaya za walengwa kutohudhuria uhakiki kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya walengwa kuhamia mashambani kwa shughuli za kilimo na hivyo kutopatikana wakati wa uhakiki," alisema Selemani.

Alisema miradi mbalimbali ya sekta za maji, elimu na afya huibuliwa na vijiji vya walengwa kwa lengo la kuboresha huduma za sekta hizo kwa jamii.

"Tofauti na vipengele vingine vya mpango, miradi hii haizinufaishi kaya za walengwa tu badala yake kila kaya kwenye kijiji/mtaa husika ina fursa sawa ya kunufaika kupitia miradi hiyo," alisema Selemani.

Alisema kuwa halmashauri za mkoa zimetekeleza jumla ya miradi 81 ikiwa ni pamoja na 28 ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, ofisi za walimu na vyoo, mradi mmoja wa ujenzi wa jengo la utawala, 23 ya ujenzi wa nyumba za watumishi, miradi tisa ya ujenzi wa mabweni, mmoja wa ujenzi wa jengo moja la huduma za uzazi, 17 ya ujenzi wa zahanati, mmoja wa ujenzi wa jengo la kufulia na ununuzi wa mashine ya kufulia na mmoja wa maji.

"Miradi hii imegharimu jumla ya Sh. 5,789,805,122.87 ambapo miradi 78 imekamilika na mitatu ipo kwenye hatua za ukamilishaji," alisema Selemani.

Hata hivyo, selemani alisema wanakabiliwa na tatizo la baadhi ya walengwa kushindwa kuhudumia miradi waliyoanzisha hasa ya ufugaji kutokana na uzee na maradhi.

HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa kanda wa kampuni ya konyagi (TDL), Davis Deogratius (kulia), akigongeana glasi za kinywaji na Meneja Mauzo Kanda ya Kusini, Mwesige Mchuruza (katikati) na Meneja wa Fedha, Fredy Kayanda, wakati wa hafla ya kusherehekea miaka 50 ya kampuni hiyo, iliyofanyika Chang'ombe jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **ICHA: MPIGA PICHA WETU**

# TFS kugawa mamilioni ya miche kwa wananchi

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu (TFS), umesema utagawa miche milioni 2.5 kwa wananchi na taasisi za serikali kwa ajili ya kuipanda kwenye maeneo yao katika Wilaya ya Songea.

Akizungumza baada ya kutembelea kitalu cha miche ya miti cha TFS kilichopo katika milima ya Matogoro, wilayani humo, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololeti Mgema, alisema lengo ni kuunga juhudi za serikali za uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na tatizo la mabadiliko ya tabianchi.

Mgema, alizitaka taasisi zote za serikali pamoja na wadau wa mazingira kuhakikisha kazi ya upandaji miti kwenye maeneo yote wilayani humo kwa kipindi hiki cha mvua inafanyika kikamilifu.

"Wakati tunakuja kukagua katika vitalu hivi ambavyo tayari vimeshaandaliwa kwa ajili ya kupandwa, nitoe wito kwa taasisi za umma, Magereza, Jeshi la Wananchi katika kila kikosi, zichukue miti na zikapande katika maeneo ambayo yameandaliwa kwa ajili ya kupanda miti hiyo," alisema Mgema.

Aliwaagiza pia wakurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea na Madaba, kuhakikisha wanahamasisha upandaji wa miti angalau milioni 1.5 kila mwaka na kuisimamia itunzwe ili ikue na kustawi vizuri.

"Kila mwaka, kila halmashauri ipande miti milioni 1.5, sisi katika Wilaya ya Songea tunazo halmashauri tatu na kila moja lazima ibebe jukumu hilo la kupanda na kutunza miti," alisema Mgema.

Kamishna Mkuu wa TFS, Profesa Dos Santos Silayo, alisema TFS imekuwa ikigawa wastani wa miche milioni 12 kwa mwaka kwa wananchi na taasisi katika wilaya na mikoa mbalimbali nchini na kuongeza mashamba yanayomilikiwa na serikali na kusaidia kupanua wigo wa upatikanaji wa malighafi ya mazao ya misitu.

"Nitoe wito kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma, wote wajitokeze katika kipindi hiki cha msimu wa mvua kuchukua miche na kupanda katika maneo yao," alisema Profesa Silayo.

"Ni matumaini yangu kwamba jitihada zilizofanywa na TFS katika ukanda huu wa Kusini ambako taarifa inaonyesha kwamba kuna miche takribani milioni nne ya kupanda katika maeneo mbalimbali ambayo inatolewa bure kwa wananchi wa mikoa hii, wajitokeze sasa kutumia fursa hii."

Mhifadhi Mkuu wa Wilaya ya Songea wa TFS, Issa Mlela, alisema kitalu hicho cha Matogolo kina miche ya aina mbalimbali ikiwamo ya vyanzo vya maji na miti ya kibiashara ambayo ikipandwa itakuwa na manufaa kimazingira na kiuchumi.

"Kitalu hiki cha Matogolo ndicho kinahudumia wilaya zote zilizopo katika Mkoa wa Ruvuma, na zimekuwa zikichukua na kwenda kugawia wananchi wao," alisema Mlela.

# Wamsimamisha mbunge wao aone walivyojitolea ujenzi

**Na Dinna Stephano,** TARIME

WANANCHI wa Kijiji cha Nyagisya, Kata ya Kiore, wamesimamisha msafara wa Mbunge wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara, kuendelea na safari wakimwomba akaone walivyojitolea nguvu zao kuchimba msingi ili kujenga zahanati.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), alikutana na wananchi hao jana alipofanya ziara kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa jimboni kwake.

Wananchi hao walikuwa wamesimama katikati ya barabara wakiwa wamebeba vifaa vya ujenzi walivyokuwa wakivitumia kuchimba msingi hali iliyomlazimu Mbunge Waitara kushuka kwenye gari kuwasikiliza.

"Mbunge wetu, mbunge wetu, tunaomba twende ukaone wananchi tulivyoamua kujitolea kujenga zahanati twende twende," walisikika wakipaza sauti zao.

Baada ya ombi hilo Waitara alikubali na kuongozana na wananchi kwa kutembea mwendo wa kilomita moja kwenda kuona msingi huo.

Walipofika katika eneo inapotarajiwa kujengwa zahanati hiyo, walimwonyesha matofali 3,500 waliyoyanunua kwa fedha zao na kuchimba msingi kwa nguvu zao hali iliyomfurahisha na kuamua kuwachangia Sh. milioni tano kwa ajili ya kununua mifuko ya saruji.

"Nawaomba wataalamu msaidie ujenzi ukamilike siyo wamalize kujenga halafu mnawaambia wabomoe kuwa ujenzi uko chini ya kiwango, nawapongeza sana kwa uamuzi mzuri na mimi nachangia milioni tano ya saruji naombeni mwendelee na moyo huo huo wa kuchangia maendeleo," alisema Waitara.

Mmoja wa wananchi hao, Anna Wang'anyi, alisema wameamua kujenga zahanati kwa kuwa wamekuwa wakiteseka kutembea umbali mrefu zaidi ya kilomita mbili kwenda kupata huduma za afya katika zahanati ya Mtana iliyopo Kata ya Manga.

Alisema wananchi wengine wanapokosa nauli ya pikipiki hulazimika kwenda Hospitali ya Wilaya ya Tarime kwa kutembea umbali wa zaidi ya kilomita tano kwa miguu.

"Zahanati ikijengwa itatusaidia sana tukienda kliniki zahanati ya Mtana, wauguzi wanatupa maneno ya kejeli ikiwamo kututaka tujenge zahanati yetu," alisema Wang'anyi.

Katarina Charles aliongeza: "Ukienda Mtana kama ujauzito wako ni wa kwanza wanakwambia hawahudumii mimba ya kwanza uende hospitali ya wilaya, ukijifungua unaombwa Sh. 10,000 hadi 20,000, tumefurahi sana kuanzisha zahanati hapa ni karibu, umbali umechangia baadhi ya wagonjwa kupoteza maisha kwa kukosa huduma ya haraka," alisema Katarina.

Waitara katika ziara yake, aliongozana na maofisa wa Idara ya Elimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime na viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa Wilaya ya Tarime.

# Apongeza ving'amuzi kupunguza ajali barabarani

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MWENYEKITI wa umoja wa usafirishaji abiria Mkoa wa Njombe, Daniel Hatanaka, amesema ufungaji ving'amuzi kwenye magari yaendayo mikoani umesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali za barabarani.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza na Nipashe kuwa king'amuzi hicho hufungwa kwenye gari na kupata mawasiliano kati ya gari, mwenye gari, LATRA na Jeshi la Polisi, kitengo cha usalama barabarani.

"Kufungwa kwa ving'amuzi kumesaidia kwa asilimia kubwa kupunguza ajali nchini hata mkoani kwetu hivyo niipongeze serikali kwa hatua hii kubwa, lakini tu waongeze juhudi katika kuvisimamia kwa sababu usimamizi wake si mzuri sana," alisema Hatanaka.

Alisema, baadhi ya madereva bado wakaidi wawapo barabarani na kuomba elimu iendelee kutolewa zaidi ili kuepuka ajali zinazosababishwa na uzembe.

Aliipongeza serikali mkoani Njombe kwa jitihada za utengenezwaji wa miundombinu ya barabara ambayo imesaidia kupunguza gharama ya uendeshaji.

Naye mratibu wa mabalozi wa usalama barabarani Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Festo Mamboleo, alisema tangu ving'amuzi vimeletwa vimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza ajali ikilinganisha na siku za nyuma ajali za mabasi zilikuwa nyingi.

"Yaani kwa asilimia 95 ving'amuzi vimesaidia kupunguza ajali," alisema Mamboleo.

Mamboleo alisema kutokana na matokeo hayo chanya anaishauri serikali magari yote yaendayo wilayani yafungwe ving'amuzi ili kupunguza ajali.

Kwa upande wake dereva David Mwakyusa alisema ajali zimepungua baada ya serikali kufunga ving'amuzi na hata madereva wameongeza umakini ili ajali zisitokee.

Nipashe
# Spotika



WAFUNGAJI 10 BORA LIGI KUBWA 5 ZA ULAYA 2020 UK. 12-13



AUBAMEYANG

# NYOTA WA5 WALIOSHINDWA KUNG'ARA EPL 2020-21

## ISIKUPITE

TANGU alipocheza kwa mara ya kwanza msimu huu kuanzia Novemba 26, Emile Smith Rowe, amehusika moja kwa moja katika mabao sita kwa Arsenal kwenye mashindano yote (mabao mawili, pasi za mwisho nne). Ni Alexandre Lacazette pekee (mabao sita, pasi moja ya mwisho) ambaye amehusika zaidi kwenye mabao mengi katika kipindi hicho ndani ya klabu hiyo.




**LONDON,** England

HUKU mwaka 2020 ukiwa haupo tena na sisi, Ligi Kuu England imeendelea kuwa katika nusu yake kwa sasa. Matokeo mengi yasiyotarajiwa yamejitokeza.

Huku Ligi Kuu ikiendelea kuwa ya ushindani mkubwa, tumeshuhudia kiwango bora kutoka kwa wachezaji.

Hata hivyo, wachezaji wengi wameshindwa kuwa kwenye ubora wao msimu huu. Makala haya inawaangalia wachezaji watano ambao wameshindwa kung'ara msimu huu, twende sasa...

### #5. ADAMA TRAORE

Mmoja wa wachezaji wenye kasi zaidi duniani, Adama Traore alikuwa kwenye kiwango bora zaidi msimu uliopita. Alitoa pasi za mwisho tisa na alifunga dhidi ya timu kubwa kama Manchester City na Tottenham Hotspur. Na hilo likamwezesha hata kupata nafasi kwenye kikosi cha timu ya Taifa ya Hispania katika mechi za Ligi ya Mataifa ya UEFA.

Traore amekuwa hayupo kwenye kiwango kabisa msimu huu, akiwa hajafunga bao wala kutoa pasi za mwisho kwenye mchezo wowote wa mashindano kwa Wolves. Traore amecheza katika kila mechi za Wolves msimu huu na ameanza katika mechi tisa, lakini bado hajafungua akaunti ya mabao kwenye Ligi Kuu England.

Traore alianza msimu kwa kuwa kwenye kikosi cha kwanza cha Wolves, lakini baadaye akawa akitumika akitokea benchi nafasi yake ikichukuliwa na Pedro Neto, hadi pale Raul Jimenez alipoumia.

### #4. MASON GREENWOOD

Mason Green alitabiriwa na wachambuzi wengi kama mmoja wa wachezaji bora vijana duniani msimu uliopita. Na kinda huyo kutoka akademi ya Manchester United, alichukuliwa kama mchezaji bora zaidi kijana kwa mwaka 2020. Alifunga mabao 10 kwenye Ligi Kuu na mchango wa mabao 24 katika mashindano yote msimu uliopita.

Greenwood alifunga mabao nane kwenye ligi mwaka 2020, lakini amefunga moja tu msimu huu. Tangu kuanza kwa msimu mpya, Greenwood amekuwa kwenye wakati mgumu wa kufunga, bao pekee alilofunga kwenye ligi msimu huu ni dhidi ya West Ham. Katika mashindano yote, amefunga mabao matatu na hajaweza kutoa pasi ya mwisho yoyote kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Ukichukulia kwamba, Manchester United ni timu ya pili kwa kufunga mabao mengi zaidi kwenye Ligi Kuu England, Greenwood anaonekana kutokuwa kwenye kiwango chake.

### #3. PIERRE-EMERICK AUBAMEYANG

Kuelekea msimu huu, Aubameyang alifunga mabao 54 katika mechi 85 za Ligi Kuu kwa Arsenal. Aliwahi pia kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji bora msimu wa 2018/19 na alimaliza katika nafasi ya pili msimu uliopita. Na akapewa unahodha katikati ya msimu uliopita na alikuwa nguzo muhimu kwa Arsenal wakati wakishinda taji la FA na Ngao ya Jamii.

Wengi walikuwa na matarajio makubwa kwa Aubameyang kuendelea kuongoza kwenye safu ya mashambulizi ya Arsenal hasa baada ya kusaini mkataba mpya. Hata hivyo, msimu huu hajawa kwenye kiwango bora.

'Washikabunduki' hao wamekuwa kwenye kiwango kibovu zaidi msimu huu, huku Aubameyang akiendelea kuwa na ukame wa mabao.

### #2. KAI HAVERTZ

Kai Havertz alikuwa na wakati mzuri sana mwaka 2020 wakati akiwa kule Bayer Leverkusen. Mchezaji huyo kijana raia wa Ujerumani alifunga mabao 10 na kutoa pasi za mwisho tano katika mechi 16 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kiwango chake kikawavutia Chelsea na wakamsajili na kutua kwenye Ligi Kuu England kwa pauni milioni 72.

Havertz alitarajiwa kwamba msimu huu atang'ara zaidi kwenye Ligi Kuu England, lakini amekuwa kwenye wakati mgumu zaidi. Wachambuzi wengi wa soka wanashangaa kuona Havertz ameshindwa kuwa kwenye ubora wake msimu huu.

### #1. BERNARDO SILVA

Watazamaji wengi wa Ligi Kuu England wanaweza kukumbuka namna Bernardo Silva alivyokuwa kwenye kiwango bora msimu wa 2018/19. Ulikuwa ni msimu wa furaha kwa raia huyo wa Ureno na alipewa tuzo ya kuwa mchezaji bora wa msimu wa Manchester City. Silva alionekana kuwa ndio mrithi sahihi wa David Silva. Lakini sasa mambo hayako poa kwa Silva, kwani mabao na pasi za mwisho zimekauka kabisa kutoka kwake.

Msimu huu Silva bado hajaweza kutoa pasi ya mchango wa mabao katika mechi 16 na kusababisha kocha wake, Pep Guardiola kumweka benchi mara kwa mara.

Silva katika umri wake wa miaka 26, kwa sasa anatakiwa kurudi kwenye kiwango chake ili aweze kupata namba pale Man City na kuwa sehemu ya kikosi cha timu ya Taifa ya Ureno.

# WAFUNGAJI 10 BORA LIGI KUBWA 5 ZA ULAYA 2020



RONALDO

**LONDON,** England

MWAKA 2020 kwa uhakika kabisa uliathiriwa sana na mlipuko wa virusi vya corona na kuleta changamoto nyingi kwenye ligi kubwa duniani.

**Ligi zililazimika kusimama kwa muda kabla ya kurudishwa bila mashabiki uwanjani na hiyo ilisababisha timu kubwa na wachezaji kutokuwa kwenye kiwango chao.**

Hata hivyo, licha ya athari hiyo ya mlipuko wa virusi vya corona, wachezaji wachache waliweza kuendelea kuwa kwenye kiwango chao na kuzisaidia timu kuendelea kuwa bora.

Makala haya yanawaangalia wachezaji 10 kutoka ligi kubwa tano za Ulaya ambao walikuwa na mabao mengi mwaka 2020, hawa hapa...

### #10. LIONEL MESSI (BARCELONA) - MABAO 19

Lionel Messi alikuwa na mwaka mbaya 2020. Na hilo likaathiri mafanikio ya Barcelona, ambao walimaliza msimu bila kubeba taji lolote kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha muongo mmoja.

Messi alifunga mabao 12 kwenye Ligi Kuu msimu uliopita. Lakini licha ya kuwa na wakati mgumu, mchezaji huyo aliivunja rekodi ya Xavi ya kuwa na pasi za mwisho nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

### #9. FRANCESCO CAPUTO (SASSUOLO)- MABAO 19

Baada ya muda mwingi kucheza kwenye Ligi ya Serie B, Francesco Caputo mwenye umri wa miaka 33, alirudi uwanjani vizuri mwaka 2018, akifunga mabao 16 kwa Sassuolo.

Caputo halafu akafuatiwa na msimu bora zaidi wa 2019-20, akifunga jumla ya mabao 21 huku 13 akiyapata kwa mwaka 2020.

### #8. KYLIAN MBAPPE (PARIS SAINT-GERMAIN) - MABAO 19

Kylian Mbappe ni mmoja wa wachezaji vijana wenye kiwango bora kabisa kwenye soka kwa wakati huu. Hata hivyo, mwaka 2020 hakuwa mzuri sana kwa soka la Ufaransa.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22, alikuwa sehemu ya kikosi cha Paris-Saint Germain (PSG) kilichofika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza. Katika msimu wa 2019-20 wa Ligue 1, Mbappe alifunga jumla ya mabao 19.

### #7. ZLATAN IBRAHIMOVIC (AC MILAN) - MABAO 20

Zlatan Ibrahimovic ameonyesha umahiri wake tangu aliporudi tena kwa klabu ya AC Milan mwanzoni mwa mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, raia wa Sweden alifunga mabao kumi na kuisaidia Milan kufuzu kucheza Ligi ya Europa.

Hata hivyo, Ibrahimovic amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara, licha ya kuwa msaada mkubwa kwa Rossoneri hao.

### #6. ROMELU LUKAKU (INTER MILAN) - MABAO 22

Romelu Lukaku alikuwa na wakati mzuri zaidi pale Inter Milan akifunga mabao 35 ya Ligi Kuu baada ya kuwa na kipindi kibaya kule Manchester United.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji, alifunga mabao 34 kwenye mwanzo wake pale Nerazzurri na kuisaidia Inter kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia

Msimu huu, Lukaku ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi akiwa ametikisa nyavu mara 12 katika mechi 14 za ligi, huku akiiwezesha Inter kuendelea kuifukuzia AC Milan kileleni mwa msimamo.

Lukaku alianza mwaka mpya vizuri zaidi kwa kufunga na kutoa pasi ya mwisho wakati Inter ikiibuka na ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya Crotone.

### #5. MOHAMED SALAH (LIVERPOOL) - MABAO 23

Mohamed Salah bila shaka yoyote ni mchezaji nguzo kwa kocha Jurgen Klopp pale Liverpool ambapo walishinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu baada ya miaka 30 msimu uliopita.

Ingawa winga huyo wa Misri alifunga mabao 19 tu ya ligi msimu uliopita tofauti na mabao 32 na 22 kwa misimu miwili iliyopita.

Msimu huu, Salah inaonekana rekodi ya kufunga mabao ipo vizuri. Alianza msimu mpya kwa kufunga mabao matatu (hat-trick) dhidi ya Leeds United na amekuwa na mchango mkubwa kwa timu hiyo msimu huu.

### #4. ERLING BRAUT HAALAND (BORUSSIA DORTMUND) - MABAO 23

Erling Braut Haaland bila shaka yoyote ni straika bora zaidi kijana kwa sasa. Tangu alipoanza kwa hat-trick kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, mchezaji huyo raia wa Norway hajaangalia nyuma. Kiwango chake akiwa kule Salzburg kikamuwezesha kuhamia kwa miamba wa Ligi Kuu Ujerumani, Borussia Dortmund, ambako nako amekuwa kwenye kiwango bora zaidi.

Haaland alifunga mabao 13 ya ligi kuisaidia Dortmund kumaliza nafasi ya pili nyuma ya mabingwa Bayern Munich kwenye Bundesliga. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, ameendelea kuwa kwenye kiwango bora zaidi, akifunga mabao 10 kwenye ligi kabla ya kuumia. Kwa msimu huu, Haaland ameendelea kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi kwenye ligi.

### #3. CIRO IMMOBILE (LAZIO) - MABAO 28

Ciro Immobile pengine ni mchezaji aliyekuwa kwenye kiwango bora zaidi na klabu yake msimu uliopita, akifunga mabao 36 kwenye mashindano yote na aliisaidia Lazio kumaliza nafasi ya tatu mwenye msimamo.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 30, msimu huu wa 2020-21 pia umekuwa bora kwake akiwa ametikisa nyavu mara 10.

### #2. ROBERT LEWANDOWSKI (BAYERN MUNICH) - MABAO 32

Robert Lewandowski aliwafunika wachezaji kama Cristiano Ronaldo na Lionel Messi katika ubora kwenye soka duniani.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland, alifunga mabao 34 katika mechi 55 za mashindano yote aliyoichezea Bayern Munich na kuisaidia kutwaa mataji matatu.

Msimu huu pia umekuwa bora sana kwa Lewandowski ambaye tayari amefunga mabao 19 kwenye Bundesliga.

### #1. CRISTIANO RONALDO (JUVENTUS) - MABAO 34

Cristiano Ronaldo alikuwa na mwaka mzuri wa 2020 kwa klabu na nchi yake.

Baada ya kufunga mara 21 kwenye ligi na kuisaidia Juventus kutwaa taji lao la tisa mfululizo la Scudetto, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 na nahodha wa Ureno, anaongoza pia msimu huu kwa kutikisa nyavu mara 14.

Mapema mwaka huu, Ronaldo alifikisha mabao 100 aliyoifungia timu yake ya Taifa ya Ureno, na kuwa mchezaji wa pili duniani kufikisha idadi ya mabao hayo kwa timu ya taifa.

Ronaldo alifungua msimu wake wa 2021 kwa kufunga mabao mawili dhidi ya Udinese.

## Nukuu

"Mwaka wa tatu kwa mkopo? Hapana, lengo langu ni kurejea Real Madrid na kuwa muhimu kwenye klabu bora duniani. Ninaamini kwamba siku moja nitarudi na kuweza kuonyesha mapenzi ambayo mashabiki walinionyesha. Kwa sababu mbalimbali, sikuiacha klabu kwa njia bora," **kiungo anayeichezea Arsenal kwa mkopo akitokea Real Madrid ya Hispania, Dani Ceballos.**




"Kama akiondoka sioni tatizo, Grealish anaweza kuziba vizuri sana pengo lake. Kundoka kwake si tatizo kwa Manchester United, Grealish ana kiwango bora kabisa kama Messi [Lionel] na Ronaldinho," **beki wa zamani wa Man United, Rio Ferdinand akiamini kwamba hata kama Paul Pogba ataondoka United majira ya joto, kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish anaweza kusajiliwa kuzipa pengo lake.**



"Mwanzoni nilikuwa nasema nitastaafu karibuni, lakini sasa nafikiria nitastaafu nikiwa mkubwa. Sijui nini kitatokea, lakini naona kabisa kwamba, siwezi kustaafu hivi karibuni kama nilivyokuwa ninawaza mwanzo," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**



# SIMBA BABA LAO CAF KWA AFRIKA MASHARIKI



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone, akichanja mbuga kuelekea lango la FC Platinum kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Januari 6, mwaka huu na Simba kushinda 4-1. **PICHA: MAKTABA YETU**

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeweka rekodi ya kuwa timu pekee kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini imeweka rekodi ya kuwa timu iliyotinga kwenye hatua hiyo mara nyingi zaidi nchini Tanzania.

**Simba ilitinga hatua hiyo Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kwa kuitwanga FC Platinum ya Zimbabwe mabao 4-0, ikitinga kwa jumla ya mabao 4-1, baada ya kufungwa bao 1-0 ugenini na nyumbani kushinda 4-0.**

Simba kwa sasa si kama itaiwakilisha Tanzania tu, bali ukanda wote wa Afrika Mashariki kwa sababu hakuna timu yoyote kutoka Kenya na Uganda, Burundi na Rwanda ambazo zimeingia hatua hiyo.

Rekodi zinaonyesha kuwa hii ni mara ya tatu sasa kwa Simba kutinga hatua hiyo, baada ya kufanya hivyo mara ya kwanza mwaka 2003 na kurudia mwaka 2018, kabla ya kufanikiwa tena kutinga mwaka huu. Makala haya, tunaiangalia safari ya Simba ilipokuwa ikianza hadi kutinga hatua ya makundi mara zote tatu na timu ambazo ilicheza nazo.

**LIGI YA MABINGWA 2003**
**SIMBA 1-0 BDF XI**

Hii ilikuwa safari ya Simba kuelekea kutinga hatua ya makundi mwaka 2003, ilipocheza hatua za awali dhidi ya BDF XI ya Botswana. Katika mechi ya kwanza iliyochezwa nchini Tanzania, Simba ilishinda bao 1-0.

**BDF XI 1-3 SIMBA**

Simba ilifunga safari na kwenda nchini Botswana kwenye mechi ya marudiano. Ilikuwa huko, iliwashangaza wenyeji wao kwa kuwatwanga mabao 3-1 na kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

**SANTOS 0-0 SIMBA**

Ilipangiwa na Santos ya Afrika Kusini na mechi ya kwanza ilichezwa Sauzi, timu hizo zikatoka suluhu.

**SIMBA 0-0 SANTOS (9-8 PENALTI)**

Mechi ya marudiano nchini Tanzania, timu hizo pia zilitoka pia suluhu na kubidi zipigiane mikwaju ya penalti. Simba ilishinda kwa penalti 9-8 na kuwenda raundi ya pili.

**SIMBA 1-0 ZAMALEK**

Ni raundi ambayo Simba ilipambana na bingwa mtetezi wa Afrika, Zamalek na kwenye mechi ya kwanza nchini Tanzania, Simba ilishinda bao 1-0.

**ZAMALEK 1-0 SIMBA (2-3 PENALTI)**

Mechi hii ya kihistoria kwa Simba ilifanyika nchini Misri, Simba ikifungwa bao 1-0, hivyo matokeo ya jumla kuwa bao 1-1 na kulazimika kupigiana penalti. Juma Kaseja aliokoa penalti mbili, na penalti ya mwisho iliyoivua ubingwa Zamalek na kuipeleka hatua ya makundi Simba, ilipigwa na Christopha Alex Massawe. Simba ikatinga hatua ya makundi, ikapangwa Kundi A, ikiwa na timu za Enyimba ya Nigeria, Ismaily ya Misri na ASEC Mimosas. Iliishia hatua hiyo baada ya kushika nafasi ya tatu.

**LIGI YA MABINGWA 2018/19**
**SIMBA 4-1 MBABANE SWALLOWS**

Ulikuwa ni mwaka wa pili kwa Simba kuweka rekodi ya kutinga makundi na ilianza dhidi ya timu ya Eswatini, Mbabane Swallows nchini Tanzania, Simba ikishinda mabao 4-1 kwenye hatua ya awali ya michuano hiyo.

**MBABANE SWALLOWS 0-4 SIMBA**

Simba ilikwenda kufanya unyama kwenye mechi ya marudiano na kuitandika timu hiyo mabao 4-0 na kuingia kwenye raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**NKANA FC 2-1 SIMBA**

Kwenye raundi ya kwanza, ilisafiri hadi nchini Zambia kucheza dhidi ya Nkana FC. Kwenye mechi hiyo, Simba ilichapwa mabao 2-1 na ikawa kama imejiweka kwenye mazingira magumu ya kutinga hatua ya makundi.

**SIMBA 3-1 NKANA FC**

Baada ya miaka 15, Simba iliweka rekodi na kutinga hatua ya makundi, ikiingia kwa mara ya pili kwa kuitandika Nkana FC mabao 3-1 kwenye mechi iliyochezwa nchini Tanzania kwa mabao ya Jonas Mkude, Meddie Kagere na Clatous Chama.

Ilipangwa Kundi D, ikiwa pamoja na timu za Al Ahly ya Misri, JS Saoura ya Algeria, na AS Vita ya Congo DR. Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali baada ya kushika nafasi ya pili kwenye kundi hilo.

**LIGI YA MABINGWA 2020/21**
**PLATEAU 0-1 SIMBA**

Baada ya mwaka mmoja tu wa kukosa kutinga hatua hiyo ya makundi ilipotolewa dhidi ya UD Songo kwa bao la ugenini, ikitoka suluhu ugenini na kutoka sare ya bao 1-1 nyumbani, Simba haikufanya makosa hayo tena, ilipoanza hatua ya awali kwa kucheza dhidi ya Plateau ya Nigeria. Kwenye mechi ya kwanza ikiwa ugenini, ilishinda 1-0 bao likifungwa na Clatous Chama.

**SIMBA 0-0 PLATEAU**

Kwenye mechi ya marudiuano nchini Tanzania, Simba ilibanwa mbavu na kutoka suluhu, lakini ilifanikiwa kutinga mbele kwa bao 1-0 na kutinga raundi ya kwanza ya michuano hiyo.

**FC PLATINUM 1-0 SIMBA**

Ikiwa nchini Zimbabwe, Simba ilichapwa bao 1-0 na timu ngumu ya FC Platinum na kujiweka kwenye mazingira magumu ya kusonga mbele, kutokana na kuhitaji zaidi ya bao moja na kutoruhusu kufungwa bao lolote kwenye mechi ya marudiano.

**SIMBA 4-0 FC PLATINUM**

Kwa namna ya kushangaza, Simba ilipata ushindi mnono wa mabao 4-0 kwenye mechi ngumu ya marudiano dhidi ya wapinzani wao FC Platinum na kutinga hatua ya makundi na tayari imepangwa Kundi A, ikiwa pamoja na mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al Merrikh ya Sudan.

**JE, WAJUA?**



MCHEZAJI wa Manchester United, Scott McTominay, hadi sasa amefunga mabao manne katika mechi 22 msimu huu, ikiwa ni pungufu ya bao moja ukilinganisha na alivyofanya msimu wa 2019-20 (mabao matano katika mechi 37). Mabao matatu kati ya hayo amefunga katika dakika tano za mwanzo za mechi hizo.



# 'Dodoma ni mwendo wa miti 10 kwa wiki kila mtu'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amekerwa na kasi ndogo ya upandaji miti mkoani humo, huku akiagiza kila mtumishi kwenye mamlaka za serikali za mitaa kupanda miti 10 kwa wiki.

Dk. Mahenge alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akiongoza upandaji miti katika eneo la Medeli jijini hapa.

Alisema kila halmashauri inapaswa kuainisha eneo ambalo lipo kwenye mpango wa kupandwa miti ili kila atakayepanda iwekwe lebo kuonyesha jina la aliyepanda.

"Pia itaonyesha taasisi ambayo imepanda, na ni wajibu wa aliyepanda kuitembelea na kuitunza kwa hiyo miti hiyo 10 mtakubaliana aidha kupanda Jumamosi ambayo ndiyo siku tuliyokubaliana kupanda miti asubuhi, lakini kwa kuwa utakuwa umepewa na mkurugenzi utapanda hata Jumatatu ukitoka kazini," alisema.

Aliongeza kuwa agizo hilo litaingizwa kwenye taratibu za nidhamu ili kila mmoja awajibike.

"Watu hawafuatilii mgawanyo wa kazi hata leo hawajaja, sasa hata kama hawajafika watambue kuwa wana miti yao 10 ya wiki hii na ijayo," alisema.

Aliuagiza uongozi wa Jiji la Dodoma kuandaa eneo kubwa ambalo zitaitwa taasisi mbalimbali kupanda kwa siku moja miche milioni 10.

"Mwaka jana tulikaa na kutengeneza andiko na kugawana maeneo, lakini utekelezaji wake upo chini sana watu wanadhani mabadiliko ya kuifanya Dodoma iwe nzuri na kuvutia itafanywa na mtu mwingine sio wao," alisema na kuongeza kuwa Dodoma kuwa ya kijani inategemea uwajibikaji wa kila mmoja na si kundi fulani.

"Tumechukulia suala la kupanda miti kama sherehe hadi aje kiongozi ndiyo tunajitokeza kupanda miti mmoja mmoja na zoezi linakufa, hatuwezi kwenda na utaratibu huu ni wajibu wetu kuibadilisha Dodoma," alisema.

Alibainisha kuwa mwaka 2006 iliagizwa kila halmashauri ipande miti 1,000,000, lakini haijawahi kufikiwa kwa kupandwa wala kufanya tathmini ya iliyopandwa.

"Mkurugenzi kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya mmesema kuna maeneo mmeainisha ya upandaji miti, basi yabandikwe kwenye kila taasisi ili kujua yale yanayopaswa kupandwa mwaka huu," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema kwa kutambua umuhimu wa mazingira jiji limejiwekea sheria ndogo zinazowataka wananchi wote wanaomiliki ardhi kupanda miti mitano kwenye maeneo yao pamoja na maeneo ya taasisi za umma ili kuliweka jiji katika mazingira pendezeshi.

"Sheria ndogo za utunzaji na usimamizi wa mazingira ya Jiji la Dodoma zimesambazwa katika kata na mitaa ili kudhibiti mifugo inayokula miti inayokua na uvamizi wa jamii kwenye misitu ya asili," alisema.



Wafanyabiashara wa matunda na mboga katika soko la Sabasaba jijini Dodoma, wakizoa taka ngumu na kuziweka kwenye kizimba kwa ajili ya kuzihifadhi na kusafirisha eneo maalumu lililotengwa kwa ajili ya dampo la kudumu la Chidaya. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waziri Afya asisitiza maadili kwa watumishi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, ameagiza vyama, mabaraza na bodi za kitaaluma nchini kusimamia maadili na weledi kwa watumishi wa sekta ya afya ili kuboresha utoaji huduma kwa wananchi.

Waziri Gwajima alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa vyama, mabaraza na bodi za kitaaluma jijini hapa.

Aliwaambia ndiyo wasimamizi wakuu na wadhibiti wa maadili na weledi kwa kuwa wananchi bado wanakutana na kero nyingi za maadili na weledi wanapopata huduma za afya.

Alisema katika ziara walizofanya kwenye mikoa mbalimbali wanakutana na kero zitokanazo na kufifia kwa maadili na weledi wa utendaji.

"Haya yote yanadhibitiwa na vyama, bodi na mabaraza ya kitaaluma, ili tuweze kuhuisha hayo yote, lazima tukae pamoja na kuangalia mifumo yao ya utendaji kazi ukoje hadi unatoa mianya ya baadhi ya wanataaluma kukosa maadili na kuleta malalamiko mengi kutoka kwa wananchi?" Alihoji.

Aidha, Dk. Gwajima alisema kutokana na malalamiko hayo inaonekana kukosa meno ya vyama hivyo vya kitaaluma.

"Kikao hiki kikubwa ni kuambiana ukweli na kuwakumbusha majukumu yao na wafahamu kuna tatizo kwa wanataaluma wanachama wao ndiyo maana hawashtuki na hata wengine kuvunja maadili bila kujali kama kuna mabaraza ya kitaaluma na kubadilika ili kuondoa kero kwa wananchi," alisema.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Dk. Godwin Mollel, alisema wataalamu wengi hivi sasa hawafanyi kazi kwa kuzingatia maadili na kusababisha makosa mengi ya kitaaluma kufanyika kwenye vituo vya kutolea huduma.

"Tunakuta makosa kwenye taaluma mfano dawa zinaibiwa, lakini wewe mwenye baraza lako hili hivi hujioni kwamba na wewe unatakiwa kuadhibiwa?" Alihoji.

# Ataka vijana kupewa elimu ya biashara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Fatma Toufiq, ameiomba serikali kutoa elimu ya usimamizi wa fedha za mikopo inayotolewa kwa halmashauri ili kuvipa vikundi vya wajasiriamali wanawake, vijana na wenye ulemavu, kuepusha kutumika kinyume na malengo na taratibu.

Toufiq aliyasema hayo wakati akifungua warsha ya vijana iliyoandaliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Endless Success Foundation yenye lengo la kuwainua vijana kiuchumi na kuacha dhana potofu ya kusubiri kuajiriwa.

Alisema serikali imeweka utaratibu mzuri wa kutoa mikopo kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, lakini kundi la vijana wengi wanashindwa kuitumia mikopo yao vizuri kwa sababu ya kutokuwa na elimu ya biashara na matumizi ya fedha.

"Ifike wakati vijana wapatiwe elimu ili kujiinua kibiashara hasa ukizingatia taifa lipo kwenye uchumi wa kati, vijana wanapaswa kuelimika kibiashara ili wasonge mbele katika biashara waliyokusudia kufanya," alisema Toufiq na kuongeza kuwa elimu hiyo itasaidia vijana wengi kunufaika na mikopo hiyo.

"Lengo la serikali ni kuona makundi ambayo imeyalenga katika mikopo yanapiga hatua kufanya maendeleo na si kurudi nyuma," alisema na kuongeza kuwa ni vyema kuwapo na mtaala wa elimu ya biashara kuanzia shule za msingi ili kusaidia kupanua uelewa kwa jamii na kujiajiri.

"Elimu ya biashara ikianzia shule ya msingi itawajengea wanafunzi ya kuchagua nini afanye pale atakapohitimu masomo yake," alisema.

Mkurugenzi wa Endless Success Foundation, Amina Feruz, alisema lengo la warsha hiyo ni kutoa elimu kwa vijana ya namna watakavyojiajiri wenyewe ikiwamo kusimamia mpango wa fedha wanazokopeshwa katika vikundi vyao.

Aliwaambia washiriki kuwa taasisi yao inalenga kuona vijana wanaachana na fikra za kusubiri kuajiriwa pale wanapohitimu masomo na badala yake wajiajiri wenyewe kupitia fursa zilizopo kwenye maeneo yao.





# Wafugaji warejesha mifugo Bonde la Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

KIWA imepita miaka 13 tangu serikali iendeshe operesheni ya kuondoa mifugo kwenye ardhi oevu ya Bonde la Ihefu, wilayani Mbarali, mkoani Mbeya, baadhi ya wafugaji wamerejesha makundi ya mifugo hiyo na kuhatarisha mazingira ya bonde hilo.

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, ililazimika kutumia ndege ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), mwishoni mwa wiki na kubaini uwapo wa makundi makubwa ya mifugo ndani ya bonde hilo ambalo ni miongoni mwa vyanzo vya maji ya Mto Ruaha.

Baada ya kujionea uhalifu huo, kamati hiyo iliitisha kikao cha dharura kilichowahusisha wawakilishi wa chama cha wafugaji, maofisa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na viongozi mbalimbali wa serikali kwa ajili ya kujadiliana namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

Akizungumza kwenye kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliwataka wafugaji waliovamia eneo hilo kuondoa mifugo yao ndani ya siku sita, baada ya hapo serikali itawachukulia hatua kali za kisheria. Alisema baada ya siku sita serikali itavielekeza vyombo vya ulinzi na usalama kufanya operesheni ya kuikamata mifugo hiyo na kuitaifisha kwa mujibu wa sheria za nchi.

"Swageni mifugo hiyo kuipeleka kule mlikoitoa, nimeona kuna athari nyingi za kimazingira ndani ya bonde hilo, baada ya siku sita kupita nitaelekeza wanajeshi, polisi, magereza, uhamiaji na migambo kufanya operesheni," aliagiza Chalamila.

Akitoa taarifa ya hali ya uhalifu wa mazingira mbele ya kamati hiyo, Mhifadhi Mwandamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Sharif Abdul, alisema takwimu zinaonyesha kuwa Wilaya ya Mbarali inaongoza kwa uhalifu wa kuingiza mifugo kwenye hifadhi ikilinganishwa na wilaya zingine zinazozunguka hifadhi hiyo.

Alisema katika wilaya hiyo wapo wafugaji wengi wakorofi ambao wanakamatwa na mifugo ndani ya hifadhi na kutozwa faini kwa mujibu wa sheria, lakini wanarudia mara kwa mara.


"Baadhi ya wafugaji hao wametozwa faini zaidi ya mara tatu wengine mara mbili, lakini hawaachi, hifadhi hii inazungukwa na wilaya za Chunya, Mbarali kwa Mkoa wa Mbeya, Iringa Vijijini kwa Mkoa wa Iringa na Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, lakini Mbarali imekuwa ni shida zaidi," alisema Abdul.

Baadhi ya wafugaji hao waliahidi kutii agizo la kuiondoa mifugo ndani ya bonde hilo huku wakiiomba serikali kuzielekeza mamlaka za vijiji kutenga maeneo ya kutosha kwa ajili ya malisho, ili kuepusha migogoro ya mara kwa mara na hifadhi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wilayani humo, Matagri Mbigili, alisema vijiji vingi vimetenga maeneo kwa ajili ya kilimo, makazi na vyanzo vya maji, lakini havijatenga maeneo ya malisho.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Mbarali, Hashim Mwalyawa, aliomba serikali iwagawie wafugaji maeneo ambayo hayafikiwi na wanyamapori ili wayatumie kwa ajili ya malisho.

Mwaka 2007 serikali iliendesha operesheni ya kuondoa mifugo ndani ya Bonde la Ihefu na kuipeleka katika mikoa ya Lindi na Mtwara pamoja na maeneo mengine nchini, lakini baadhi ya wafugaji wamerejea tena.



Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel (kushoto), akisalimiana na mkalimani wa lugha ya alama wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, Faraja Mbwilo, alipofanya ziara katika hospitali hiyo, kulia ni Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mvua yaleta madhara, yakosesha makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MVUA inayoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali mkoani Mbeya, imeleta madhara kwa kusababisha watu kukosa makazi baada ya kutokea kwa mafuriko yaliyosababisha nyumba kubomoka na zingine kujaa maji.

Nipashe lilishuhudi nyumba nyingi zikiwa zimezingirwa na maji kwenye maeneo ya Uyole, Nzovwe na Kalobe jijini hapa, pamoja na mitaa mbalimbali ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Baadhi ya nyumba kwenye kitongoji cha Songambele, Kata ya Utengule Usongwe, Mbalizi, chemchemi za maji zimetokea na kusababisha baadhi ya nyumba kubomoka.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wananchi wa kitongoji hicho, Chibhili Mtafya, alisema mafuriko hayo yameleta madhara makubwa kwenye nyumba yake pamoja na za majirani.

"Mwaka jana madhara yalitokea kwenye choo changu ambacho kilibomoka, lakini mwaka huu naona hatari zaidi maana maji yametokea chumbani ninakolala na nina wasiwasi nyumba inaweza ikabomoka," alisema Mtafya.

Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Akson, ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, alifanya ziara katika maeneo ya jiji hilo yaliyokumbwa na mafuriko kwa ajili ya kuwafariji waathirika.

Akiwa katika mtaa wa Majengo Mapya, aliahidi kumsaidia mmoja wa wazee Tamali Mgema, kusafisha nyumba yake ambayo mafuriko yalileta matope na kuharibu kila kitu kilichokuwamo, huku akiahidi kumsaidia chakula.

"Kuna vijana watakuja hapa watakusaidia kusafisha nyumba yako na watakuletea na chakula, lakini tutaendelea kuwasaidia na wengine ambao wamepata madhara kutokana na mafuriko haya," alisema Dk. Tulia.

# Wenye ulemavu wa kusikia kusaidiwa dawa kufubaza VVU

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ZAIDI ya watu 20 wenye ulemavu wa kusikia wanaoishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi (VVU) mkoani Mbeya, wameingizwa kwenye mpango wa matumizi ya dawa za kufubaza virusi hivyo, baada ya Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kuajiri mkalimani wa lugha ya alama.

Kuajiriwa kwa mkalimani huyo kunaeleza kuchochea kundi hilo kujitokeza kupata huduma za matibabu katika hospitali, kutokana na kuondoa tatizo la ugumu wa mawasiliano kati yao na wataalamu wa afya. Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa hospitali hiyo, Dk. Godlove Mbwanji, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ya kukagua maendeleo ya taasisi mbalimbali za afya mkoani humo. Alisema tangu walipomwajiri mkalimani huyo zaidi ya wenye ulemavu huo 300 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakihudhuria katika hospitali hiyo kupata huduma za kiafya ambazo walikuwa wanashindwa kuzipata kabla.

"Watu hawa wamehamasika sana kuja kupata huduma za matibabu baada ya kubaini kwamba huduma ya mkalimani wa lugha ya alama yupo hapa na wanaeleza kabisa kuwa wanafurahia hii huduma," alisema Dk. Mbwanji.

Alisema waliamua kuajiri mtaalamu huyo baada ya kubaini kuwa kuna tatizo la mawasiliano kati ya madaktari na wenye ulemavu huo hali ambayo ilikuwa inazorotesha huduma hiyo.

Naibu Waziri Dk. Mollel alipongeza uongozi wa hospitali hiyo kwa ubunifu walioufanya huku akieleza kuwa hospitali zingine nchini zinatakiwa kuiga ili kuwasaidia walemavu hao kupata huduma.

Alisema pamoja na ushauri huo kwa hospitali zingine, lakini serikali italifanya jambo hilo kuwa la kisheria na kisera ili litekelezwe kwa ufanisi nchi nzima na liwe jambo la lazima. Aliushauri uongozi wa hospitali hiyo kuwa na mawasiliano na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), ili kushirikiana kwenye utoaji wa baadhi ya matibabu makubwa yakiwamo ya moyo, ili kuwasaidia wananchi kupunguza gharama za kuyafuata matibabu hayo jijini Dar es salaam.

Vilevile, alisema serikali inakusudia kuzifanya hospitali zote za kanda nchini kuwa na uwezo wa kutoa matibabu ya kibingwa kama ilivyo MNH. "Kwa sasa zaidi ya nchi 18 barani Afrika wananchi wake wanakuja kutibiwa MNH, sasa tunataka tuziboreshe na hizi hospitali za kanda zihudumie na nchi jirani, hospitali hii ya Kanda ya Mbeya inahudumia mikoa nane tunataka ihudumie hata watu kutoka Malawi, Zambia na DRC," alisema Dk. Mollel.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR), Kituo cha Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Elias Nyanda, alisema taasisi hiyo inafanya utafiti ambao utawezesha kuboresha vipimo na matibabu ya ugonjwa wa kifua kikuu.

Alisema wanafanya utafiti ili kubaini kama inawezekana kupima ugonjwa huo kwa kumpima mgonjwa damu, mkojo na choo pamoja na kupunguza dozi ya tiba ya ugonjwa huo ambayo kwa sasa mgonjwa anameza vidonge kwa muda wa miezi sita.





# Mwinyi awataka Wazanzibari kuwa wakarimu kwa wageni

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka Wazanzibari kuendelea kudumisha amani na utulivu na kuwa wakarimu kwa wageni.

Amesema kwa kufanya hivyo kutawatengenezea mazingira mazuri wageni wanaofika visiwani humo kurejea tena.

Alitoa rai hiyo juzi wakati wa ufunguzi wa hoteli ya Le Mersenne Beach Resort, iliyo katika mradi wa "Jumeira Holdings Company Ltd" iliyopo Michamvi, Wilaya ya Kusini, Mkoa wa Kusini Unguja.

Akiwa katika ufunguzi huo, Dk. Mwinyi aliwapogeza wananchi wa Zanzibar kwa kuwakaribisha vyema wageni na kuwataka kuendelea kudumisha amani na utulivu, ili watalii wandelee kuiona Zanzibar ni kisiwa cha amani.

Katika hotuba yake Dk. Mwinyi aliuhimiza uongozi wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na wadau wengine kuongeza kasi ya kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya.

Vile vile, Dk. Mwinyi alihimiza umuhimu wa kuendeleza utalii unaozingatia uhifadhi wa mazingira.

Dk. Mwinyi alitoa shukrani na pongezi kwa wawekezaji wa hoteli hiyo kwa uamuzi wao wa busara wa kuichagua Zanzibar katika kuwekeza na kwamba hatua hiyo itasaidia kutekeleza lengo la serikali la kutengeneza ajira 300,000.

Pia, Dk. Mwinyi alisema mradi huo umetoa ajira kwa wananchi 103 katika nafasi mbalimbali na idadi hiyo itaongezeka wakati hoteli hiyo itakapokuwa inapokea wageni wengi zaidi.

Alisema amefurahi kuona wawekezaji wa mradi huo wanaendelea kukamilisha taratibu zitakazowawezesha kutekeleza mradi mwingine mkubwa katika kisiwa cha Pemba.

Alieleza hatua hiyo inaendana na dhamiraya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kukifanya Kisiwa cha Pemba kuwa eneo maalum la uwekezaji, kuitaka ZIPA kuhakikisha kwamba zoezi hilo linakwenda vizuri.

Dk. Mwinyi alisema kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejielekeza katika kuendeleza uchumi wa buluu, ambao umejumuisha sekta ya utalii.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Soraga, alisema kufunguliwa kwa hoteli hiyo yenye hadhi ya nyota tano ni miongoni mwa adhma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kupokea watalii wa daraja la juu, ambao watakuza hadhi ya nchi kiutalii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Salum Khamis Nassor, alisema mradi huo unaendeshwa na kampuni ya Jumeira Holding Ltd.

Alisema mradi huo ulianzishwa Machi 15, 2011 ukiwa na mtaji wa makisio wa Dola za Kimarekani milioni 8.4.

Alisema hadi kufikia Desemba, mwaka jana, ZIPA imeidhinisha miradi 761 ya uwekezaji yenye mtaji wa makisio wa Dola za Kimarekani bilioni 7.3 katika sekta ya utalii.

Mwekezaji wa hoteli hiyo, Riaz Mawani, alimpongeza Dk. Mwinyi kwa kushinda uchaguzi na kuwa Rais wa Zanzibar na kueleza matumaini ya wawekezaji kutokana na kasi yake.

Mmiliki huyo alieleza azma yake ya kushirikiana na serikali katika kutekeleza Ilani ya CCM katika kuwasaidia vijana kupata ajira, vijana 103 wamepata ajira.



Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Abdallah Hussein Kombo, akizungumza na waandishi wa habari jana, baada ya kufungua semina ya siku mbili kuhusu umuhimu wa sekta ya uvuvi, kwa vijana 70, iliyoandaliwa na Taasisi ya Mimi na Mwinyi ikishirikiana na ushirika wa Wakulima Hai Co-operative Society iliyopo Zanzibar. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Wajasiriamali wataka utatuzi kero usafirishaji bidhaa nje

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI kutoka visiwani Zanzibar wameziomba taasisi zinazosimamia usalama wa chakula na vipodozi kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wakati wanaposafirisha bidhaa kwenda nje.

Waliyasema hayo wakati wa kikao kati yao na Viongozi wa Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), kilichohusu mchakato wa kuingia makubaliano na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

Katibu wa jumuiya ya wasafirishaji bidhaa nchi za nje, Khamis Issa, alilalamikia hatua ya vitambulisho vya kusafirishia bidhaa vinavyotolewa na ZBS na ZFDA kutotambulika na Tanzania Bara. Alisema kuna usumbufu mkubwa wanaoupata wajasiriamali wa Zanzibar wanapohitaji kupeleka bidhaa za nje jambo linalosababisha baadhi yao kukata tamaa.

Hivyo, alizitaka ZBS na TBS kukaa pamoja, kushirikiana na kuaminiana katika kujenga umoja na ushirikiano wa pande mbili za Muungano ili kutatua matatizo hayo.

Mjasiriamali kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara Wanawake Zanzibar (ZWCC), Zeyana Ahmed Kassim, alisema TBS imeandaa mazingira ya kuwasaidia wajasiriamali wa Tanzania Bara, lakini mpango huo haupo kwa Zanzibar.

Alisema hali hiyo husababisha baadhi ya wajasiriamali kutoka Zanzibar kuomba kujiunga na TBS, ili kuepukana na usumbufu wakati wanaposafirisha bidhaa zao. Kwa upande wake Mkurugenzi ZFDA, Bora Lichanda, alisema lengo la ZFDA ni kuwaondolea vikwazo wanavyokabiliana navyo katika kutekeleza shughuli zao bila kupata usumbufu kama wanavyodai.

Hivyo, aliahidi kuyafayia kazi mapendekezo yaliyotolewa na wajasiriamali hao kabla ya mchakato wa kuingia makubaliano na TBS kufanyika.

# Watumishi afya, benki watakiwa kuwajali wazee

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Abdullah Juma Mabodi, ameitaka jamii, watumishi wa sekta za kutoa huduma ikiwamo afya, benki kuwaheshimu wazee, kwa kuwa wanamchango mkubwa katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aliyasema hayo wakati wa zoezi la kupima afya kwa Baraza la Wazee waliopo katika jimbo hilo, ikiwa ni maandalizi ya sherehe za miaka 57 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Alisema wazee wa Zanzibar wanahistoria kubwa katika nchi ikiwamo kujitolea katika kuleta maendeleo katika nyanja tofauti.

Alisema wazee hao wakati wa ujana wao walishiriki kikamilifu shughuli zote za kuleta maendeleo Zanzibar katika afya, elimu, makazi na hata utunzaji wa mazingira katika maeneo yao.

Alisema ni vyema kuwatizama na kuhakikisha wanapewa huduma zote zinaostahiki ikiwamo chakula, malazi bora, pamoja na kuwashughulikia afya zao.

"Wazee ndio hazina yetu hatuna budi kuwatunza kwa kuwapatia mambo yote yanayostahiki kupatiwa kama walivyotuhudumia sisi walijitolea kwa kiasi kikubwa ili kuhakikisha jamii inapata maendeleo, sasa ni wakati wetu sisi kujitolea kwa wao ili na wao wajisikie fahari, alisema Juma Mabodi.

Alisema Rais Dk. Husein Mwinyi ameahidi kuendeleza na kuwaenzi wazee kama walivyofanya watangulizi wake, kwa kuwa wao ndiyo hazina kubwa nchini.

Naye Mbunge wa jimbo hilo, Mwanakhamisi Kassim, alisema wazee wanahitaji huduma bora ya afya ikiwamo kufanya vipimo mara kwa mara pale wanapohisi mabadiliko katika miili yao.

Alisema serikali itaendelea na zoezi la kuwajali wazee katika nyanja mbalimbali ikiwamo afya ili kuhakikisha wanaishi bila ya hofu.

Akisoma risala ya Baraza la Wazee, Katibu wa Baraza hilo, Maryam Haji Shehe, alisema wamekuwa na utaratibu wa kuwapima afya wazee wote waliofikisha miaka 60 kila mwaka.

# Wananchi hatarini daraja kuchakaa

**Na Idda Mushi,** MLIMBA

WANANCHI wa VIjiji vya Tanganyika, Kata ya Masagati na Mfenesi wako katika hatari ya kukosa mawasiliano ya barabara kutokana na daraja la mbao wanalolitegemea kuvuka kuchakaa na baadhi ya mbao na magogo kukatika na kushindwa kupitisha magari.

Daraja hilo lililoshikiliwa na magogo ya miti linaunganisha vijiji vya Tanganyika na Mfenesi, vyenye huduma za shule ya msingi, makanisa, zahanati pamoja na vijiji vingine vya Taweta na Masagati katika kata ya Masagati.

Pia maeneo mengine ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, kikiwamo Kituo cha Afya cha Mlimba ambacho wajawazito hutegemea upasuaji kwenda kufuata huduma.

Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Tanganyika, January Amos na Hilda Malinda, walisema daraja hilo licha ya kutumika kuvuka, wanalitegemea kuvusha mazao na kufuata huduma zingine za kijamii.

"Changamoto nyingine ya eneo hili ni uotaji wa majani yanayosababisha kuziba barabara, hivyo tunawaomba TARURA (Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini) kuhakikisha fedha wanazotoa mwanzoni mwa mwaka, mwezi Julai, zinaletwa Machi ili kusaidia na usafi wa barabara hii ambayo kipindi hicho hufungwa na majani na kugeuka kuwa kama kichochoro," alisema January.

Diwani wa Kata ya Masagati, Blasius Makao, alisema licha ya hatari ya daraja hilo, wana tatizo pia la kujaa maji kwenye kipande cha barabara kinachounganisha daraja kuelekea Tanganyika na wakati wa msimu wa mvua wananchi wanatumia mitumbwi kufika kijijini na kuomba eneo hilo la barabara kulazwa kifusi.

Baadhi ya kinamama akiwamo Railoda Kilangavana, mkazi wa Kijiji cha Taweta, wamekiri wajawazito kufariki njiani kutokana na kukwama magari wakiwa wanafuata huduma za rufani kutokana na ubovu wa barabara na kuiomba serikali kufanyia matengenezo kipande cha kutoka Kata ya Masagati hadi Mlimba.

Mbunge wa Mlimba, Godwin Kunambi, alisema baada ya kupokea taarifa ya hatari ya daraja hilo, alianza kutafuta msaada wa dharura wa matengenezo kutoka kwa Mtendaji Mkuu wa TARURA, Meneja wa Mkoa na wa Wilaya ili kupata msaada wa haraka na akashukuru kukubali kujenga upya daraja hilo.

Kunambi alisema iwapo hatua za haraka zisingechukuliwa, kungekuwa na madhara makubwa ikiwamo watu kuangukia mtoni na kupoteza maisha.

"Usafiri pekee uliobaki kwa sasa ni wananchi kutumia pikipiki ama kutembea kwa miguu wakati wakisubiri kutengenezwa kwa daraja, na tunashukuru serikali kupitia TARURA wamesikia kilio hiki na kutenga Sh. milioni 53 ili kujenga upya daraja hilo kwa kiwango cha miti na nataka ndani ya muda mfupi wawe wamekamilisha," aliongeza Kunambi.

Meneja wa TARURA Wilaya ya Kilombero, Mhandisi Robert Magogo, alisema wameanza maandalizi ya ujenzi wa daraja hilo ikiwamo kuandaa magogo na mbao msituni ili kujenga upya daraja hilo.

Alisema ujenzi huo utakwenda sambamba na ujenzi wa kilometa tatu na nusu za barabara na tayari kampuni ya Gramemo LBT, imekabidhiwa kuianza kazi hiyo inayotegemewa pia kutumia nguvu kazi ya wananchi wa maeneo husika.



Daraja linalokatiza Mto Mfuji linalounganisha vijiji vya Tanganyika Kata ya Masagati na Mfenesi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba wilayani Kilombero, ambalo limechakaa na haliwezi kupitika hasa kwa magari, litajengwa upya na TARURA kwa bajeti ya dharura kunusuru usalama wa watumiaji. **PICHA: IDDA MUSHI**

# TANESCO lawamani huduma umeme

**Na Neema Hussein, RUVUMA**

MKUU wa Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, Cosmas Nshenye, amewataka wafanyakazi wa Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) wilayani humo, kuwasilisha ripoti zao ofisini kwake kila mwezi, kwa madai ya kukithiri kwa uzembe na kushindwa kujisimamia.

Aidha, Mwenyekiti wa CCM Mbinga, Beda Hyera, amedai kuwa shirika hilo linaongoza kuwatesa wananchi wa Mbinga kutokana na kukithiri shida ya kukatika umeme mara kwa mara kwa wastani wa mara 15 hadi 20 kwa siku.

Nshenye kwa upande wake aliwataka waache kufanya kazi kwa mazoea, wajielekeze kutatua kero na kuboresha huduma zao kwa wateja ikiwamo kumaliza tatizo sugu la kukatika umeme.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC), kilichofanyika Mbinga.

Alidai, shirika hilo linaonekana kushindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na huduma mbovu linazotoa kwa wananchi ikiwamo kushindwa kuwaunganishia umeme licha ya kulipa gharama kwa wakati.

Alisema kama watumishi wa shirika hilo wameshindwa kufanya kazi kwa ufanisi wajiondoe Mbinga ili waje watu wengine ambao wako tayari kuhudumia wananchi.

"Kuna malalamiko mengi ofisini kwangu juu ya tabia yenu mbaya ya kuchukua fedha za watu, lakini mnashindwa kuwapatia huduma, nimechoka kusikia malalamiko dhidi yenu, kuanzia sasa nataka kila mwezi mlete taarifa ya utendaji wenu ofisini kwangu maana wenyewe mmeshindwa kujisimamia," aliagiza Mkuu wa Wilaya.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa CCM Mbinga, Beda Hyera, alisema shirika hilo linawatesa wananchi na kama halitabadilika kiutendaji kuna hatari wananchi wakakosa imani na kuichukia serikali yao.

Aliitaka TANESCO kufuatilia makandarasi waliopewa kazi ya kusambaza umeme vijijini chini ya miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kwa madai ya kukiuka makubaliano ya mkataba kwa kuuza nguzo kwa wananchi, licha ya huduma hizo kutolewa bure.

Alidai pamoja na kuwachukulia fedha kwa ahadi ya kuwaunganishia umeme majumbani, hawafanyi hivyo.

Vile vile, alilalamikia kitendo cha makandarasi wa REA kupeleka umeme katika vijiji vilivyopo pembezoni mwa barabara kuu na kuviacha vijiji vya pembezoni.

Mwenyekiti wa CCM, alimtaka Meneja wa TANESCO na timu yake kuwafuatilia mara kwa mara makandarasi wa REA wanaofanya kazi ya kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti vitendo vya utapeli kwa wananchi.

Mbunge wa Mbinga Mjini, Jonas Mbunda, alizitaka taasisi za serikali likiwamo Shirika hilo kutoa huduma bora kwa wananchi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwa kuwa tabia hiyo inarudisha nyuma mipango mizuri ya serikali.

# Aonya makandarasi kujaa vijijini

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

MBUNGE wa Mkuranga mkoani Pwani, Abdallah Ullega, amesema makandarasi wengi wanaofanya kazi vijijini, hawana uwezo na kusababisha kazi nyingi kukwama.

Ullega ambaye ni Naibu Waziri wa Habari na Michezo, aliyasema hayo kwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Afya, Mapato na Miundombinu, Dk. Festo Dugenge, wakati alipotembelea Mkuranga na kukagua miundombinu, mapato ya Hospitali ya Mkuranga na ujenzi wa barabara.

Ullega alisema, baadhi ya makandarasi wanashindwa kufanya kazi wakati wengine walitaka wapatiwe pesa kwanza ndio wafanye kazi.

"Makandarasi inatakiwa wafanye kazi sio kutanguliza pesa mbele kinachotakiwa ni kuwa wazalendo katika kufanya kazi na kuwa wakweli," alisema Ullega.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Filbeto Sanga, alisema miundombinu ya barabara Mkuranga, inatatizo kubwa na kuutaka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), kuongezewe fedha.

Alisema asilimia 30 inakwenda TARURA wakati 70 inachukuliwa na Wakala wa Barabara (TANROAD).

Sanga alisema miradi mingi ya barabara inashindikana kuendelea kutokana na kutotekelezwa kwa mikataba na kwamba inatakiwa itekelezwe ikiwamo na kujengwa kwa viwango.

"Barabara zijengwe kwa viwango na sio kujengwa baada ya miezi miwili inaharibika," alisema.

HABARI KIMATAIFA

# Miili yaopolewa ufukweni ajali ya ndege

**Jakarta,** INDONESIA

SEHEMU ya miili ya watu waliopata ajali ya ndege imeopolewa katika kisiwa cha Jakarta, baada ya ndege iliyokuwa imebeba abiria 62 kuanguka muda mfupi baada ya kupaa.

Msemaji wa Polisi, Yusri Yunus, alisema, jana asubuhi, kuwa wamepokea mifuko miwili, mmoja ukiwa na sehemu ya mwili na mwingine ukiwa na mali zinazoaminika kuwa ni za abiria.

Mamlaka nchini Indonesia, ilisema rada ya kufuatilia ndege inaonyesha kuwa ndege hiyo aina ya Boeing 737-500 ilianguka baharini dakika nne, baada ya kuondoka kutoka kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa Soekarno-Hatta mjini Jakarta.

Ndege hiyo, ilikuwa inaelekea kwenye mji wa Pontianak ulio katika kisiwa cha Borneo.

Safari ya ndege hiyo ilitegemewa kuchukua muda wa dakika 90 juu ya usawa wa bahari ya Java.

**Wavuvi katika eneo lililo karibu na mlolongo wa visiwa kaskazini mwa pwani ya Jakarta, waliripoti baada ya kusikia mlipuko, saa nane na nusu mchana Jumamosi.**

Waziri wa Uchukuzi wa Indonesia, Budi Karya Sumadi, aliwaambia waandishi wa habari kuwa ndani ya ndege hiyo walikuwamo watu 62 miongoni mwao wahudumu wa ndege, ikiwamo watoto 10.

Waziri Sumadi alisema ndege hiyo ilichelewa kwa saa moja kabla ya kuruka na ilipoondoka mwendo wa saa nane na dakika 36, dakika nne baadaye, ikapotea kutoka kwenye rada baada ya rubani kutoa mawasiliano kwa kitengo cha udhibiti wa safari za anga kuwa anaruka umbali wa futi 29,000 usawa wa bahari.

Eneo linalodhaniwa kutokea ajali hiyo ya ndege ni karibu na visiwa maarufu vinavyotembelewa na watalii kando na pwani ya mji mkuu wa Indonesia, Jakarta.

Wavuvi katika eneo lililo karibu na mlolongo wa visiwa kaskazini mwa pwani ya Jakarta, waliripoti baada ya kusikia mlipuko, saa nane na nusu mchana Jumamosi.

Mvuvi mmoja aliliambia Shirika la Habari la AP kwamba waliposikia mlipuko huo walidhani labda ni bomu au Tsunami na baada ya hapo waliuona mlipuko mkubwa kutoka baharini.

Mamlaka imeweka vituo viwili vya kushughulikia yanayohusiana na ajali hiyo, kimoja kwenye uwanja wa ndege na kingine kipo bandarini.

Familia zimekusanyika katika vituo hivyo kusubiri taarifa za wapendwa wao.

Kwenye mitandao ya kijamii, watu walianza kutoa taarifa za ndege hiyo nambari SJ-182 ya shirika la ndege la Sriwijaya Air, picha na video za watu waliorodheshwa kama abiria kwenye ndege hiyo.

Moja kati ya video hizo inamwonyesha mwanamke na watoto wake wakipunga mikono ya kwaheri katika uwanja wa ndege kabla ya kuondoka.

Mkurugenzi wa shirika hilo la Sriwijaya, Jefferson Irwin Jauwena, aliwaambia waandishi wa habari kwamba ndege hiyo iliyohudumu kwa miaka 26.

Alisema awali ndege hiyo, ilitumiwa na mashirika ya ndege ya Marekani, haikuwa na matatizo yoyote na kwamba kabla ya kupata ajali siku hiyo, ilikuwa tayari imefanya safari kwenda katika miji ya Pontianak na Pangkal Pinang.

Indonesia, taifa lenye watu milioni 260, linasifika kuwa na idadi kubwa ya visiwa duniani mara kwa mara, hukumbwa na ajali zinazohusisha vyombo vya usafirishaji wa ardhini, baharini na angani. Inadaiwa ni kutokana na miundombinu chakavu na viwango duni vya usalama katika sekta ya usafiri. **DW**

## Burundi yafunga mipaka kudhibiti maambukizi corona

**Bujumbura,** BURUNDI

SERIKALI ya Burundi, imetangaza kuwa itafunga mipaka yake ya majini na ardhini kuanzia leo, ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya corona ambayo yameonekana kuongezeka wiki iliyopita.

Hatua hiyo ni baada ya wiki iliyopita watu zaidi ya 40 kuambukizwa virusi hivyo ndani ya siku mbili katika nchi hiyo.

Aidha, serikali nchini humo, imetangaza kuwa abiria wote watakaowasili nchini humo kwa ndege, watalazimika kukaa karantini kwa muda siku saba na wakipatikana na virusi hivyo, watapelekwa katika vituo maalum kwa gharama zao.

Agizo hili jipya limetolewa na Waziri wa Usalama, Gervais Ndirakobuca, wakati nchi hiyo ikiwa na maambukizi 884 ya corona tangu kisa cha kwanza kilichoripotiwa mwaka uliopita. Hata hivyo, wadadisi wa mambo wanasema kuwa huenda nchi hiyo ikapata maambukizi makubwa kutokana na idadi ndogo ya upimaji wa virusi hivyo. **RFI**

## Watoto 10 wafariki dunia kwa moto

**Maharashtra,** INDIA

WATOTO wachanga 10 wamefariki katika moto wakiwa kwenye kitengo cha wagonjwa mahututi cha hospitali katika Jimbo la Maharashtra, India.

Ilibainika kuwa watoto saba, waliokolewa katika moto huo, maofisa wa polisi wamebaini kuwa moto huo unaweza kuwa ulianza kwa sababu ya mzunguko mfupi katika umeme.

Imerekodiwa kuwa watoto waliokufa walikuwa na umri wa miezi mmoja hadi mitatu. **TRT**



Kiongozi wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, akizungumza na shirika la habari la Italia kuwaonya wananchi wanaokataa kupata chanjo ya virusi vya corona, kwamba wanaweka rehani maisha yao na wengine. Mwanzoni mwa wiki ijayo atapata chanjo hiyo. **PICHA FP**

## Kim atoa vitisho kuimarisha zaidi nyuklia

**Pyongyang,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un ametangaza orodha ya mifumo ya teknolojia ya hali ya juu inayoendelea, akitishia kuimarisha ghala la silaha za nyuklia.

Kulingana na ripoti ya Shirika la Habari la Korea (KCNA), Kim Jong-un, ambaye alizungumza katika kongamano la nane la Chama cha Wafanyakazi wa Korea, lililofanyika katika mji mkuu Pyongyang baada ya miaka mitano, alisema kuwa Korea Kaskazini iko wazi kufanya mazungumzo na Washington, lakini Marekani lazima iongeze zaidi uwezo wake wa kijeshi na nyuklia ili kukabiliana na uhasama wake.

Alisisitiza katika hotuba yake kwamba Marekani ni adui mkuu wa Korea Kaskazini, aliongeza kwa kusema;

"Yeyote atakayechukua madaraka nchini Marekani hatabadilisha muundo wa kimsingi na sera ya uhasama ya nchi hiyo."

Alibainisha kuwa kuanzisha uhusiano mpya na Marekani kunategemea iwapo Washington itashikilia sera yake ya uhasama.

Kim alisema silaha za nyuklia hazitatumika isipokuwa pale vikosi vya maadui vitakapojaribu kutumia silaha za nyuklia.

Wakati wa ufunguzi wa Bunge, Kim alikiri kwamba karibu sekta zote za nchi zilibaki nyuma ya mipango ya maendeleo ya uchumi, na kwamba mpango wa maendeleo wa miaka mitano, uliowekwa mwaka 2016 na haukufaulu.

Akizungumzia shida zinazokabiliwa na utawala wake kama mbaya zaidi na zisizotarajiwa, Kim alitaka kutengenezwe mpango mpya wa miaka mitano. **TRT**

## HABARI MICHEZO




# NEUER AWEKA REKODI MBOVU BUNDESLIGA

**MUNICH,** Ujerumani

GOLIKIPA wa Bayern Munich, Manuel Neuer, ameweka rekodi ya kufungwa mechi nyingi zaidi kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Kwa mara ya kwanza kwenye maisha yake ya soka, Neuer ameruhusu kufungwa mabao katika mechi 10 mfululizo.

Neuer amecheza Bundesliga kwa miaka 15 sasa na hajawahi kuruhusu mabao kwa michezo 10 mfululizo, huu ni msimu mbaya zaidi kwa golikipa huyu mwenye umri wa miaka 34.

Bayern Munich walianza mchezo dhidi ya Borussia Mönchengladbach kwa kuongoza 2-0 kabla ya Mönchengladbach kupindua meza na kushinda 3-2.

# Klopp atoa darasa Liverpool kupambana

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Jurgen Klopp, amewataka wachezaji wake wapambane dhidi ya dunia, huku akisisitiza kwamba timu yake kuwa chini ya kiwango katika mechi za hivi karibuni, hakumuumizi kichwa.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England, hivi karibuni waliambulia pointi mbili tu kati ya tisa ambazo wangeweza kuzipata kwenye mechi tatu na kuiacha vita ya ubingwa kuwa wazi.

Huu umekuwa ni msimu wa tofauti kwa Klopp ambaye kwa sasa hana mabeki watatu wa kati chaguo la kwanza ambao ni majeruhi.

Klopp anafanya mazungumzo na wamiliki Fenway Sports Group, kuhusu changamoto wanazotakiwa kuzikabili katika kipindi cha pili cha msimu, lakini amejikita katika kuzungumza na wachezaji wake kuwaongezea morali.

"Katika nyakati njema kila mtu hufikiri wamiliki ni watu wazuri sana," alisema Klopp.


"Katika nyakati mbaya, kila mtu anafikiri ni wagumu sana. Wanaifuatilia sana klabu, mafanikio ya klabu na jinsi tunavyoyapata.

"Shabiki anaweza akaamini tunahitaji beki wa kati, lakini kazi yangu ni kuwafanya imara iwezekanavyo wachezaji tulionao hapa.

"Je, beki mmoja wa kati anaweza kumaliza matatizo yetu yote? Klabu inajaribu kufanya inachoweza, lakini kama hawawezi tunapaswa kufanya kile tulichokifanya hadi sasa, kuwa imara kama kundi.

"Kubaki pamoja na kupambana dhidi ya dunia. Kupambana dhidi ya mazingira yote. Kujibu mashambulizi ya maneno yao kwa kuufanya msimu huu kuwa maalum zaidi ya yote. Hivyo sasa, wakati kila mtu anafikiri 'sasa hawana nafasi', tunawaonyesha kuwa tunayo." alisema Klopp.





# *Ibrahimovic sasa kurejea uwanjani*

**MILAN,** Italia

NYOTA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, anaweza kuichezea timu yake hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kukosa mchezo dhidi ya Juventus.

Mchezaji huyo huyo mwenye umri wa miaka 39, alikuwa na kiwango bora msimu huu, akifunga mabao 10 katika mechi sita.

Lakini, Ibrahimovic alipata maumivu ya nyama za paja baada ya kufunga bao lingine la ushindi wa 3-1 dhidi ya Napoli Novemba 22, na kumfanya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Kocha wa Milan, Stefano Pioli, aliwaambia waandishi wa habari Ijumaa kuwa hakutarajia mchezaji huyo wa zamani wa kimataifa wa Sweden atarudi, lakini aliorodheshwa katika kikosi cha watu 24 kilichoorodheshwa kwenye tovuti ya Milan siku ya mchezo.

Rossoneri ambao ni vinara wa Serie A, walipata kipigo cha kwanza cha ligi msimu huu nyumbani kwa Juventus katikati ya wiki, mabingwa watetezi wakishinda 3-1 wakati Federico Chiesa alifunga mara mbili.

# Mourinho kumvuta Perisic Tottenham

**LONDON** England

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo kwenye mchakato wa kufanya mazungumzo na Inter Milan juu ya mkataba wa mkopo kwa winga, Ivan Perisic.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alirudi San Siro msimu uliopita baada ya kumaliza msimu wa mkopo na Bayern Munich, lakini ameanza kwenye nusu tu ya mechi 22 za Inter msimu huu.

Kulingana na chapisho la Foot Mercato, Inter wako tayari kumtoa Perisic kwa mkopo kwa nusu ya pili ya msimu wa 2020-21 na Spurs ni miongoni mwa timu zinazovutiwa na huduma yake.

Jose Mourinho anasemekana kuwa anamkubali sana mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia na ana matumaini ya kufanikisha makubaliano kabla ya dirisha kufungwa hapo Februari Mosi, mwaka huu.

Perisic, ambaye yuko chini ya mkataba na Inter hadi 2022, ana bao moja na pasi za mwisho mbili katika mechi 15 za kampeni Serie A msimu huu. Huenda akatua Tottenham ikiwa watakamilisha dili hili.



# MKHITARYAN APEWA MKATABA MPYA ROMA




**ROME,** Italia

NYOTA wa AS Roma, Henrikh Mkhitaryan, anaripotiwa kuwa amekubali kusalia klabuni hapo hadi mwishoni mwa msimu ujao.

Nyota huyu wa zamani wa Arsenal na Manchester United, amekuwa akifanya vema kwenye kikosi hicho cha kocha, Paulo Fonseca na amecheza kila mechi ya Serie A msimu huu, akifanikiwa kuona nyavu mara nane na kutoa pasi za mwisho saba.

Mkhitaryan amesaini mkataba mpya na Roma unaomfanya aendelee kuwapo klabuni hapo.

Nyota huyo alifika klabuni hapo kwa mkopo akitokea Arsenal dili lake likiwa linamalizika mwaka 2021, lakini kutokana na ubora wake, Roma bado wanaihitaji huduma yake.

Kwa mujibu wa mtaalamu wa masuala ya uhamisho, Fabrizio Romano, pande zote zimeshakubaliana juu ya suala la kuongeza mkataba wa nyota huyu hadi mwaka 2022.

Mkhitaryan, licha ya kuwa na mchango wa moja kwa moja kwenye mabao 15 ya ligi, pia amechangia bao moja na pasi mbili za mwisho kwenye Ligi ya Europa. Jumla ana mabao 18 na pasi za mwisho 15 tangu alipohamia Roma.

# *Lampard afunguka ugumu kazi ya ukocha*

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema kuwa aliamua kuingia Chelsea akitambua mahitaji ya klabu, alitarajia kuwa kutakuwa na shinikizo kubwa katika kusaka mafanikio na alitambua kuwa kazi hiyo haitakuwa rahisi.

Kocha huyo amesema Chelsea wanapofanya vibaya inakuwa inafurahisha zaidi na inampa fursa ya kujifunza zaidi.

"Natakiwa kusema kuwa nilikuja kwenye kibarua hiki nikitarajia msukumo na kwa upande wangu niliona kama mambo yakiwa yanaenda vema, nahitaji kujipa shinikizo mwenyewe ili kuhakikisha napata matokeo bora zaidi kwa upande wangu," alisema Lampard.

Lampard amesema kuwa klabu ina matarajio makubwa na analitambua hilo, na hiyo ndiyo sababu kubwa inayomfanya avutiwe zaidi kufanya kile ambacho anakifanya, anafurahia zaidi kwa kuwa anapenda kile anachokifanya.

"Sikutarajia kama nitakuwa na kazi rahisi baada ya kuingia kwenye klabu kubwa ya soka ambayo inajijenga kuwa bora zaidi, nilitarajia changamoto nyingi," alisema Lampard.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# ZIDANE NA MATUMAINI RAMOS KUBAKI MADRID

## ●●● Ninachotaka na tunachotaka tayari unajua, utaniuliza tena kwenye mkutano mwingine wa...

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane anatumai suala la mikataba ya Sergio Ramos na Lucas Vazquez na Real Madrid "litatatuliwa".

**Ramos mwenye umri wa miaka 34 na Vazquez, 29, wote mikataba yao inamalizika mwishoni mwa msimu na hatima yao klabuni hapo bado haina uhakika.**

Ripoti zinaonyesha Ramos amekataa mkataba wa mwaka mmoja kutoka Madrid, klabu aliyoanza kuitumikia tangu mwaka 2005.

Alipoulizwa kuhusu Ramos na Vazquez pengine wasisaini mikataba mipya, Zidane aliwaambia waandishi wa habari: "Sitaki lakini, katika mpira wa miguu, huwezi kujua.

"Ninachotaka na tunachotaka tayari unajua. Utaniuliza tena kwenye mkutano mwingine wa waandishi wa habari baada ya mechi na nitakuambia kitu kimoja. Ninatumaini ni kwamba hii litatatuliwa, hakuna zaidi."

Madrid ambao juzi, Jumamosi waliwakaribisha Osasuna kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na kutoka suluhu, wanatafuta kuwapa presha Atletico, ambao wako mbele kwa alama mbili na wana mechi mbili mkononi.

Mustakabali wa Eden Hazard tena ni gumzo huko Madrid na mchezaji huyo alianza mchezo wa ligi Novemba.

Lakini Zidane hayuko tayari kujihatarisha na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, ambaye amekuwa akipambana na majeraha tangu alipowasili klabuni hapo.

"Yuko pamoja nasi. Anafanya mazoezi mara kwa mara, halafu baada ya hapo sijui," alisema.

## ZISIKUPITE

### MILAN YAMTAKA LINGARD

INTER Milan inamtaka kiungo wa Manchester United na England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 kwa mkopo, lakini inaweza kumtoa kiungo wake Christian Eriksen, 28. ***(Sunday Mirror)***

### POCHETTINO AMWANIA POGBA

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 27, anatakiwa na kocha mpya wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino. ***(Daily Star Sunday)***

### UPAMECANO ATAKIWA CHELSEA

KLABU ya Chelsea imeripotiwa kuwania kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Dayot Upamecano mwenye umri wa miaka 22. ***(Mail on Sunday)***

### LEIPZIG KUUZA NYOTA WAKE

RB Leipzig imeripotiwa itauza wachezaji wake nyota baada ya mlinzi wake, Dayot Upamecano, 22, kuwaniwa na timu za Ligi Kuu England. ***(Manchester Evening News)***

### OZIL KUONDOKA ARSENAL

KIUNGO Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 32, yupo tayari kuondoka Arsenal ambako kwa sasa hachezi na hajacheza katika mchezo wowote huku akitajwa kuwaniwa na klabu ya Uturuki, Fenerbahce. ***(Sun on Sunday)***

### RICE HAITAKI MAN UNITED

KIUNGO wa West Ham United, Declan Rice, 21, angependa kubaki London na hana mpango wa kujiunga na Manchester United. ***(Sunday Mirror)***

### DAKA AWANIWA WEST HAM

WEST Ham imepewa ofa ya kumsajili nyota wa Red Bull Salzburg, Patson Daka mwenye umri wa miaka 22 raia wa Zambia, kwa pauni milioni 25, kama mrithi wa mchezaji wa Ivory Coast, Sebastien Haller, ambaye amejiunga na Ajax. ***(Sunday Mirror)***

### TORREIRA KWENDA FIORENTINA

KIUNGO wa Arsenal, Lucas Torreira, 24, raia wa Uruguay anaweza kuwa njiani kwenda Fiorentina, baada ya nyota huyo wa Uruguay kutofurahia maisha kule Atletico Madrid anakochi kwa mkopo. ***(Mundo Deportivo)***

### SALIBA KUSAJILIWA NICE

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Nice ipo tayari kumsajili mlinzi wa Arsenal, William Saliba mwenye umri wa miaka 19, kwa mkataba wa kudumu kipindi cha majira ya joto. ***(Sun on Sunday)***

### BROOKS AWANIWA ENGLAND

KLABU ya Aston Villa inafikiria kumsajili kiungo wa Bournemouth na Wales, David Brooks mwenye umri wa miaka 23. ***(Sunday Mirror)***

### UNITED, CAICEDO WAACHANA

KLABU ya Manchester United imeachana na mpango wa kutaka kumsajili kiungo, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ecuador. ***(Sky Sports)***

HABARI MICHEZO

## Morocco amkubali Kwizera Namungo

**Na Saada Akida,** Zanzibar

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema mshambuliaji raia wa Burundi, Eric Kwizera, atakuwa miongoni mwa usajili mpya ambao wataufanya hivi karibuni.

Akizungumza na gazeti hili jana visiwani hapa, Morocco alisema Kwizera, ambaye kwa sasa yupo kwenye majaribio na klabu hiyo inayoshiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi, ameridhishwa na kiwango cha nyota huyo, hivyo amemwingiza katika mipango yake ndani ya kikosi hicho.

Alisema mshambuliaji huyo amekuwa akifanya mazoezi na kikosi cha Namungo FC kwa muda mrefu pia amemchezesha katika mechi mbili za Kombe la Mapinduzi na kuonesha ubora wake.

"Michuano ya Mapinduzi ni sahihi kwangu katika kuwapima baadhi ya wachezaji ambao nahitaji kuwasajili akiwamo Kwizera, tayari ameanza kunishawishi.

Alisema mbali na Kwizera pia kuna wachezaji watatu wa kigeni kutoka Ghana na Cameroon wapo katika majaribio wakicheza nafasi tofauti tofauti.

## Vita Ligi Kuu Bara yahamia Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU za Simba, Yanga na Namungo, tayari zimetinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi huku Chipukizi na Jamhuri za visiwani hapa zikishuhudiwa zikiaga michuano hiyo sambamba na bingwa mtetezi, Mtibwa Sugar ya Turiani mkoani Morogoro.

Kuingia nusu fainali kwa timu hizo tatu za Bara huku Azam FC nayo jana jioni ambayo ilikuwa ikivaana na Mlandege ya visiwani hapa, ilikuwa ikipewa nafasi kubwa ya kushinda na kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo iliyoshirikisha timu tisa mwaka huu.

Timu za Bara zimeongeza mvuto mkubwa kwa mashabiki wa hapa na kila zinapocheza wamekuwa wakijazana uwanjani kuzishuhudia, hivyo nusu fainali kati ya Simba na Namungo na Yanga dhidi ya mshindi wa mechi ya jana kati ya Azam na Malindi ni mechi ambazo zitavuta mashabiki wengi zaidi visiwani hapa.

# CHAMA AWEKA REKODI SIMBA MICHUANO CAF

**Na Adam Fungamwangwo**

WAKATI Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu ya Simba, Haji Manara, akiweka kwenye mtandao wake wa kijamii picha za kiungo mshambuliaji wao, Clatous Chama akisaini mkataba wa kuichezea timu hiyo, mchezaji huyo ameingia kwenye rekodi ya kufunga mabao ya mwisho kwenye mechi ambazo timu hiyo imekuwa ikifuzu mechi za kimataifa.

**Chama amefunga mabao ya mwisho ambayo ndiyo yamekuwa yakiibeba Simba kutinga hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika pamoja na robo fainali.**

Kiungo huyo mnyumbulifu raia wa Zambia, Chama, ndiye aliyefunga bao la nne na la mwisho kwenye mechi ambayo Simba ilitinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, Simba ikishinda 4-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Februari 6, mwaka huu.

Lilikuwa ni bao la mwisho lililoipa uhakika wa asilimia zote Simba kutinga hatua ya makundi. Mabao mengine yakifungwa na Erasto Nyoni, Shomari Kapombe na nahodha John Bocco, kabla ya Chama kumalizia kazi.

Desemba 23, mwaka 2018, Chama alifunga bao dakika ya 88, kwenye uwanja huo huo wa Benjamin Mkapa wakati huo ukiitwa Taifa, lililoipeleka Simba hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, wakati ikiifunga Nkana FC ya Zambia mabao 3-1.

Kwenye mechi hiyo, Simba iliingia makundi kwa jumla ya mabao 4-2, baada ya kufungwa 2-1 nchini Zambia.

Chama aliendeleza rekodi yake hiyo Mei 17, mwaka 2019, Simba ikifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuifunga AS Vita ya DR Congo kwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Lilikuwa ni bao la Chama dakika ya 89 likiwa ni la pili, lililoipeleka Simba hatua hiyo kabla ya kutolewa kwa jumla ya mabao 4-1 na TP Mazembe ya DR Congo.

Kwa maana hiyo, ni mchezaji aliyehusika kwenye hatua zote za mafanikio ya Simba kutinga makundi mara mbili, pamoja na hatua ya robo fainali.

Mwishoni mwa mwaka jana, Mwekezaji wa klabu hiyo, Mohamed "Mo" Dewji aliwahakikishia wanachama na mashabiki wa Simba kuwa amemsajili kiungo huyo baada ya uvumi kuwa anawindwa na udi na uvumba na mahasimu wao, Yanga, kutokana na kuwa mkataba wake unakaribia kumalizika.

Pamoja na kuweka wazi, bado kumekuwa na minong'ono kwa baadhi ya mashabiki kuwa hawajaona picha ya Chama akisaini, kabla ya juzi Manara kuweka picha hizo ambazo zimemaliza kabisa uvumi huo.

WACHEZAJI BURE...




Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Elidad ya Boko Basihaya jijini Dar es Salaam, Dk. Harry Matoyo (kulia), akifafanua jambo wakati wa kutangaza kampeni ya Afya Bure kwa wanamichezo na watu wote watakaojitokeza kesho. Pembeni ni Mkuu wa Utabibu wa hospitali hiyo, Dk. Cynthia Bashaija. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Wanamichezo waitwa Hospitali ya Elidad kupimwa bure*

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU mbalimbali za soka na michezo mingine nchini, zimetakiwa kuacha kuingia gharama za kuwatibu wachezaji wao nje ya nchi kwa kuwa matibabu hayo yanapatikana hapa hapa nchini tena kwa bei nafuu zaidi, imeelezwa.

Wito huo umetolewa na mmoja wa madaktari bingwa wa mifupa nchini, Harry Matoyo, wa Hospitali ya Elidad ya Boko Basihaya jijini Dar es Salaam wakati wa akitangaza Kampeni ya Afya Bure iliyopangwa kufanyika kesho katika maadhimisho ya Sikukuu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Matoyo ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, alisema siku hiyo watatoa huduma ya vipimo bure kwa wanamichezo na wanajamii nyingine huku akijitolea kuwapima wachezaji wa timu ya Taifa, Taifa Stars ambayo inajiandaa na mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Alisema baadhi ya klabu zimekuwa na tabia ya kupeleka wachezaji walioumia nje ya nchi kama India na Afrika Kusini kupata matibabu na kuingia gharama kubwa wakati wanaweza kupata huduma hiyo hapa nchini kwa ubora uleule tena kwa bei nafuu.

Alifafanua kuwa wanaweza kuepuka gharama hizo kwa kutibiwa hapa nchini kwani hakuna haja ya kupanda ndege na kwenda kutumia gharama nyingine kubwa.

"Kutokana na hali hiyo, tumeamua kuendesha zoezi la kupima afya bure kwa wanamichezo na watu ambao siyo wanamichezo, wanawake, wanaume, wazee, vijana na watoto, mbali ya matatizo ya mifupa, pia tutapima na magonjwa mengine na kutoa ushauri wa kitabibu bila gharama zozote," alisema Matoyo.

Alisema zoezi hilo litafanyika eneo la hospitali yao Basihaya kuanzia saa 2:00 asubuhi mpaka saa 10:00 alasiri, kazi hiyo ikifanywa na madaktari.

"Lengo ni kuwawezesha kujua matatizo na aina gani ya tiba wanatakiwa kupata kutokana na matatizo hayo. Hivyo mtu yeyote anakaribishwa na tuna vifaa vya kisasa vya kufanya vipimo mbalimbali," alisema.

# Michezo

Jumatatu Januari 11, 2021

Nipashe




## Zidane na matumaini Ramos kubaki Madrid

UKURASA 22

CHA KWANZA...



Kiungo wa Arsenal, Emile Smith-Rowe, akiifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 2-0 dhidi ya Newcastle United kwenye mechi ya raundi ya nne ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Emirates juzi. Bao lingine lilifungwa na Pierre-Emerick Aubameyang. **PICHA: MTANDAO**

## Wafungaji 10 Ligi 5 bora za Ulaya 2020

**LONDON,** England

MWAKA 2020 kwa uhakika kabisa uliathiriwa sana na mlipuko wa...



HABARI UK. 12

## Lampard afunguka ukocha kazi ngumu

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard, amesema kuwa aliamua kuingia Chelsea akitambua mahitaji ya...



HABARI UK. 21

# Simba yamrejesha Morrison dimbani

## Matola achambua pia ubora wa Taddeo Lwanga, huku akitaja kurejea na Kombe la Mapinduzi...

**Saada Akida na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

BAADA ya kutoonekana uwanjani kwa muda mrefu, winga wa Simba, Bernard Morrison, amerejea na atakuwa ndani ya kikosi cha timu hiyo katika michezo ijayo ikiwamo ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea visiwani hapa.

**Morrison anarejea baada ya klabu yake ya zamani, Yanga awali kudai kuwa amezuiwa kucheza mechi yoyote ya kimashindano na Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), kutokana na kesi dhidi yao Yanga.**

Akizungumza na gazeti hili jana, visiwani hapa, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema Morrison alikuwa hayuko fiti baada ya kusumbuliwa na ugonjwa wa malaria na kumsababishia kulazwa hospitali lakini sasa amerejea kikosini na kufanya mazoezi ya nguvu na kuonyesha kurejea katika ubora wake.

"Hakuna shida yoyote zaidi ya ugonjwa ambao umemfanya asicheze, sasa yupo fiti na tutarajie kumwona katika mechi zetu zijazo atakuwamo hasa katika fainali hizi za Kombe la Mapinduzi," alisema Matola.

Kuhusu kiwango cha kiungo mkabaji wa mpya, Mganda Taddeo Lwanga, Matola alisema ni mchezaji ambaye amekuja vizuri na atakuwa msaada mkubwa kwa timu hiyo.

"Ni mechi ya kwanza kucheza, aliposajiliwa, alikuwa mgonjwa na sasa amepona na amerejea vizuri zaidi, kwa nilivyomuona nina imani kubwa ya kutusaidia na kufanya vizuri," alisema Matola.

Akizungumzia kuhusu wachezaji wapya, Bernard Agele kutoka Sudan Kusini, Kelvin Moyo na Ian Nyoni, alisema wako kwa ajili ya majaribio na wanatumia michuano ya Mapinduzi Cup kuona uwezo na ubora wa nyota hao.

"Kwa sasa ni mapema kusema lolote kwa sababu wapo katika majaribio na tutaona hadi mwisho wa mashindano haya baada ya kuridhishwa na viwango, tutaweka wazi kulingana na utaratibu wetu wa usajili," alisema Matola.

Akizungumza mechi ya juzi dhidi ya Mtibwa Sugar katika hatua ya makundi ya michuano ya Mapinduzi, Simba ikishinda mabao 2-0, Matola alisema mechi hiyo walikuwa wanataka kulipa kisasi ya finali ya mwaka jana.

"Tuliingia uwanjani tukiwa na matokeo ya fainali iliyopita, niliongea na wachezaji wangu kwa kufuata maelekezo niliyowapa na kufanikiwa kuwaondoa mashindanoni Mtibwa," alisema Matola.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanafika fainali na ikiwezekana kurejea Dar es Salaam na kombe hilo. Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Amaan juzi, mabao ya Simba yalifungwa na Hassan Dilunga dakika ya 26 na Miraji Athumani dakika ya 36.

Simba itashuka uwanjani hapo leo dhidi ya Namungo FC kwenye mechi ya nusu fainali, wakati Yanga ikitarajiwa kucheza dhidi ya mshindi wa jana usiku kati ya Azam FC na Malindi.

Kwa upande wa kocha Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Vicent Barnabas, alisema kitu ambacho kimewafanya washindwe ni kutokana na ubora wa wapinzani wao walionao msimu huu.

Alisema pamoja na kuwa mwaka jana walifika fainali, kikosi ambacho wanacho safari hii kina mabadiliko kadhaa ya wachezaji kutoka timu B ambao bado wanaendelea kusoma mazingira ya kucheza timu kubwa, hivyo uzoefu pia uliwagharimu.

9 770856 541002 >